# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

# MHE. DKT. SHUKURU JUMANNE KAWAMBWA (MB)

# AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2011/12

**Dodoma**

**Julai, 2011**

# I. UTANGULIZI

## Hoja

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusiana na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2011/12.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kuniwezesha mimi kusimama hapa mbele ya Bunge lako tukufu nikiwa na uhai na afya njema.

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda nitumie fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa tena kuongoza kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. Napenda pia kumpongeza Dkt. Mohamed Gharib Bilal kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha napenda kuchukuwa fursa hii kumshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa heshima kubwa aliyonipa kwa kuniteua kuongoza Wizara hii muhimu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na watanzania wote kwa ujumla kwamba nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kuhakikisha kuwa nafanikisha malengo ya Wizara hii na yale ya Taifa kwa ujumla. Aidha naendelea kuwashukuru wananchi wa jimbo la Bagamoyo

kwa kuendelea kuniamini kwa kunichagua kwa mara ya pili kuwa mbunge wao. Nawashukuru pia wananchi wangu wa jimbo la Bagamoyo kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu jimboni.

4. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuteuliwa na hatimaye kupitishwa kwa kura nyingi na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliopewa nyadhifa za kuongoza Wizara mbalimbali katika Serikali hii ya Awamu ya Nne katika muhula wa pili.

5. **Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa Spika na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza kuongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano. Hii inadhihirisha jinsi Waheshimiwa Wabunge walivyo na imani kubwa juu ya busara zako pamoja na uwezo na uzoefu wako katika kuliongoza Bunge letu tukufu. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Job Ndugai (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika.

6. **Mheshimiwa Spika**, natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe, Katibu Mkuu Profesa Hamisi Omari Dihenga, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Selestine Muhochi Gesimba pamoja na Kaimu Kamishna wa Elimu Bi. Marystella M. Wassena; Wakurugenzi, Viongozi wa Wakala, Mashirika, Mabaraza na Vyuo Vikuu vilivyo chini ya Wizara; Viongozi katika ngazi mbalimbali na Wafanyakazi wote, kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na maandalizi ya bajeti hii. Aidha, shukurani

zangu ziwaendee viongozi wa vyama vya wafanyakazi na vyama vya wanataaluma, kwa ushirikiano wao.

7. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuishukuru, kwa dhati, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, ikiongozwa na Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Margreth Simwanza Sitta, Mbunge Viti Maalum**, kwa kuichambua na kuijadili bajeti hii kwa kina na kisha kuyapitisha makadirio ya Wizara yangu. Napenda kulihakikishia bunge lako tukufu kwamba Wizara yangu imezingatia mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na itaendelea kupokea mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge ili kuimarisha utoaji wa elimu na mafunzo nchini.

## II. MAJUKUMU YA WIZARA

8. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekabidhiwa majukumu ya kuweka viwango vya ubora wa elimu na na mafunzo ya ufundi katika ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi; Elimu ya Sekondari; Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi; Mafunzo ya Ualimu; Elimu ya Juu, pamoja na Taasisi na Mabaraza yaliyo chini yake. Aidha Wizara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa utoaji wa elimu kwa kufanya ufuatiliaji na tathmini. Wizara pia, ina wajibu wa kufanya mapitio, kuandaa na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya sera, mipango, sheria na kanuni za elimu zilizopo, kulingana na mabadiliko ya dhima na dira ya Serikali na kuandaa mikakati ya utekelezaji wake.

## III. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2010/11 NA MATARAJIO YA MWAKA 2011/12

9. **Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kwa kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/11 na baadaye nitatoa mwelekeo wa Mapato na Matumizi ya fedha za Wizara kwa mwaka 2011/12.

### Mapato ya Mwaka 2010/11

10. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2010/11 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilipanga kukusanya maduhuli ya Serikali Shilingi bilioni **5.048.** Hadi tarehe 30 Juni, 2011; Shilingi bilioni **4.382** zilikuwa zimekusanywa.

### Matumizi ya Mwaka 2010/11

11. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2010/11, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 665.573. Kati ya hizo, Shilingi bilioni **525.941** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni **139.632** zilikuwa ni za maendeleo.

    Hadi tarehe 30 Juni, 2011, matumizi ya kawaida yalikuwa **Shilingi bilioni 503.379** na matumizi ya maendeleo yalikuwa **Shilingi bilioni 76.821.**

12. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo ya jumla kuhusu matumizi ya fedha zilizopokelewa Wizarani, ifuatayo ni taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/11.

## IV. Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/11

### Ofisi ya Kamishna wa Elimu, Idara na Vitengo vya Wizara

### Ofisi ya Kamishna wa Elimu

13. **Mheshimiwa Spika**, *Ofisi ya Kamishna wa Elimu* ina majukumu ya kuweka na kudhibiti viwango vya ubora wa elimu na utoaji wa elimu katika ngazi za Awali; Msingi; Sekondari; Mafunzo ya Ualimu; Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi; pamoja na Ukuzaji Mitaala, Uendeshaji Mitihani, Huduma za Maktaba na Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu. Ofisi ya Kamishna wa Elimu inajumuisha vitengo vya Elimu Maalumu, Elimu kwa Redio, Usajili wa Shule, Ithibati ya Vifaa vya Elimu pamoja na Masuala Mtambuko.

14. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, *Ofisi ya Kamishna wa Elimu,* pamoja na majukumu mengine, ilitekeleza yafuatayo:
    a) ilitoa vifaa pamoja na visaidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum, katika Shule za Msingi 317, za Sekondari 30 na Vyuo vya Ualimu 7;
    b) ilichagua wanafunzi wenye ulemavu 356 waliofaulu Mtihani wa Taifa wa Kuhitimu Elimu ya Msingi, kwa ajili ya kujiunga na kidato cha kwanza mwaka wa masomo 2011;
    c) ilijadili miswada *(manuscripts)* 236 ya vitabu vya kielimu kupitia Kamati ya Ithibati ya Vifaa vya Kielimu *(Educational Materials Approval Committee - EMAC)*, ambapo miswada 200 iliidhinishwa kwa masharti ya kufanyiwa marekebisho na 36 ilikataliwa;

d) ilisajili shule 169, ambapo 112 ni shule zisizo za Serikali na 57 ni shule zilizojengwa kwa nguvu za wananchi;

e) iliandaa taarifa ya awali ya mradi wa 'Utafiti kuhusu Ubora wa Elimu katika Nchi 15 za Kusini na Mashariki ya Afrika' *(The Southern and Eastern Africa Consortium for Monitoring Educational Quality - SACMEQ Research Project III)* na kutoa rasimu ya kwanza, ambapo kazi ya kuihariri inaendelea;

f) ilichambua maombi 400 ya leseni za kufundishia na kutoa leseni kwa waombaji 170;

g) iliandaa na kutangaza vipindi 528 redioni vya masomo ya Shule za Msingi; na

h) iliandaa na kutangaza vipindi 52 redioni kuhusu mbinu za ufundishaji.

## Idara ya Elimu ya Msingi

15. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, *Idara ya Elimu ya Msingi* iliendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya MMEM (2007 - 2011) kama ifuatavyo:

(a) ilikamilisha hadidu za rejea kwa ajili ya tathmini ya Awamu ya Pili ya MMEM ili kuandaa andiko la Awamu ya Tatu ya Mpango huo;

(b) iliwezesha kufanyika kwa mafunzo kwa ajili ya walimu 210 wa masomo ya Hisabati, Sayansi, English na Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kutoka Halmashauri 15;

(c) iliandaa mwongozo wa ufundishaji wa somo la sayansi kwa vitendo ambao tayari umefanyiwa majaribio.

(d) iliwezesha kufanyika kwa mafunzo ya uongozi na uendeshaji wa elimu ya msingi kwa maafisa elimu 161 kwa kipindi cha mwezi mmoja, katika Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu, (ADEM) huko Bagamoyo;

(e) iliratibu na kufuatilia utekelezaji wa 'Mpango wa Lishe Shuleni' katika Halmashauri 16 zenye ukame na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa utoaji wa huduma ya chakula shuleni. Aidha, iliandaa rasimu ya andiko *(Concept Note)* la 'Mpango wa Kitaifa wa Lishe Shuleni', na kuliwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu kwa hatua zaidi.

(f) ilifuatilia uandikishaji wa watoto katika elimu ya Msingi katika Halmashauri 30 za mikoa 10, ambapo taarifa za awali zinaonesha kuwa uandikishaji ulikuwa wastani wa asilimia 50. Aidha, iliandaa vipeperushi na mabango ya uhamasishaji juu ya umuhimu na taratibu za uandikishaji wa watoto katika elimu ya awali;

(g) iliendelea na uandaaji wa miongozo ya 'Ufuatiliaji na Tathmini ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto' na 'Upimaji wa Utoaji wa Elimu ya Awali'. Aidha, wadau 50 kutoka Halmashauri 5 za Bagamoyo, Temeke, Mtwara Vijijini, Magu, na Siha walijengewa uwezo kuhusu malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto; na

(h) iliandaa na kuratibu Mtihani wa Taifa wa Darasa la IV na kufuatilia uendeshaji wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la VII.

## Idara ya Elimu ya Sekondari

16. **Mheshimiwa Spika**, *Idara ya Elimu ya Sekondari* ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu katika ngazi ya Elimu ya Sekondari ambayo kimsingi ni kiungo kati ya Elimu ya Msingi na Elimu ya Juu. Aidha, Idara ya Sekondari inasimamia utoaji bora wa elimu kwa usawa kuanzia kidato 1– 6; na kuweka viwango na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu ya sekondari itolewayo nchini.

17. **Mheshimiwa Spika**, Elimu ya Sekondari hutolewa katika ngazi ya kawaida *(O-level)* ambayo huchukua miaka minne na ngazi ya juu *(A-level)* ambayo ni ya miaka miwili. Hadi tarehe 30 Juni, 2011, jumla ya shule zote za sekondari nchini zilikuwa 4,266. Kati ya hizo, shule 3,397 ni za serikali (3,308 za wananchi za kutwa, 89 ni shule kongwe za serikali) na 869 ni shule zisizo za serikali. Jumla ya wanafunzi katika shule za sekondari za serikali na zisizo za serikali nchini ni 1,638,699. Wanafunzi wa kidato cha 1 – kidato cha 4 ni 1,566,685 (wasichana 699,951). Wanafunzi wa kidato cha 5 na 6 ni 72,014 (wasichana 28,577). Idadi kubwa ya wanafunzi waliopo shuleni ni kielelezo cha juhudi za wananchi katika kupanua na kuendeleza elimu ya sekondari nchini.

18. **Mheshimiwa Spika**, wananchi wameendelea kuona mafanikio ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) yanayotokana na kuongezeka kwa udahili katika kidato cha 1. Katika mwaka 2010, wanafunzi waliosajiliwa katika kidato cha 1 katika shule za sekondari za serikali na zisizo za serikali walikuwa 438,827 na mwaka 2011 walikuwa 467,155

19. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kushuka kwa ufaulu katika mitihani ya Kidato cha 4, idadi kubwa ya wanafunzi waliopata daraja la I – III katika mitihani ya kidato cha 4 ambao ndiyo wenye sifa za msingi za kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha 5 mwaka 2011, wanatoka shule za sekondari za kutwa za Wananchi. Kati ya watahiniwa 38,781 waliopata daraja la I-III katika mitihani ya Kidato cha 4 mwaka 2010, wanafunzi 19,126 wanatoka Shule za Sekondari za Wananchi za Kutwa. Aidha, wanafunzi 3,697 wametoka katika shule kongwe za sekondari za serikali na 15,958 wanatoka katika shule za sekondari zisizo za serikali.

20. **Mheshimiwa Spika,** tamko la kugatua uendeshaji wa shule za sekondari lilitolewa na Mheshimiwa Rais mwezi Februari 2008. Shughuli mbalimbali za utekelezaji wa tamko hilo zilianza tangu wakati huo, na mpaka sasa Serikali inaendelea kukamilisha mchakato wa kugatua usimamizi na uendeshaji wa shule za sekondari. Ugatuaji huu ulifanyika kwa malengo yafuatayo:

(a) kusogeza usimamizi na uendeshaji wa shule karibu na wadau;

(b) kusogeza uratibu wa utekelezaji wa kila siku wa mitaala ya masomo karibu na Halmashauri; na

(c) kutoa nafasi zaidi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kusimamia na kutekeleza majukumu yake ya msingi.

21. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto zinazotokana na ugatuaji, huduma kwa walimu na wanafunzi zinafanyika kwa mafanikio zaidi sasa. Aidha, Wizara yangu inaendelea kuwa na dhamana ya Sekta ya elimu, yenye wajibu wa kutambua elimu bora kwa nchi yetu na kusimamia upatikanaji wake.

22. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2010/11, wizara yangu ilitekeleza yafuatayo:

(a) iligharimia mafunzo kazini kwa walimu 1,000 wa masomo ya sayansi, hisabati na *english;*

(b) iligharimia mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya wawezeshaji 336 wa masomo ya sayansi na hisabati kwa lengo la kuinua ubora wa ufundishaji wa masomo hayo;

(c) ilitoa kompyuta kwa ajili ya shule 30 na kuendesha mafunzo kwa walimu kuhusu namna ya kuzitumia katika kufundisha masomo anuwai kwa kupitia mtandao;

(d) iliwezesha kuanzishwa kwa vituo vya mafunzo kazini kwa ajili ya walimu wa hisabati na sayansi katika shule za sekondari 25 katika mikoa 21 na kuvipatia: vifaa vya

maabara (fizikia, kemia na biolojia), kompyuta, printa, fotokopia, skana, mashine ya kurudufia *(duplicator)* na projekta ya LCD kwa kila kituo;

(e) iliendesha kambi za sayansi kwa wanafunzi wa kike 100 kwa lengo la kuwajengea wanafunzi hao uwezo wa kufaulu masomo ya sayansi na hisabati. Aidha, ilitoa mafunzo ya kuendesha kambi hizo kwa walimu 30 wa shule za sekondari za mkoa wa Dar es Salaam;

(f) iliandaa miongozo ya kuwezesha ufundishaji wa masomo ya sayansi (fizikia, kemia na biolojia) kwa vitendo kwa kidato 1-4, ambapo nakala 5,000 zilichapishwa kwa kila somo;

(g) ilifanya tathmini na ufuatiliaji wa ufundishaji wa masomo ya sayansi na hisabati, hususan kwa walimu waliopata mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kufundisha masomo hayo, katika mikoa 10, ili kubaini manufaa na changamoto zinazotokana na utekelezaji wa mtaala;

(h) ilikamilisha utayarishaji wa Awamu ya Pili ya MMES na kuwezesha kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mnamo tarehe 19 Januari, 2011;

(i) iliandaa Mpango wa Utekelezaji na Mpango wa Ununuzi;

(j) ilitoa mafunzo kwa watendaji 527 wa Halmashauri, maafisa elimu wote wa Mikoa na wakuu wa Shule 903 ili kuwaelimisha juu ya utekelezaji wa MMES Awamu ya Pili;

(k) ilitoa vivunge vya sayansi *(Science Micro Kits)* vyenye vifaa vinavyoweza kutumika katika majaribio ya masomo ya fizikia, biolojia na kemia kwa ajili ya shule za sekondari 180 katika mikoa tisa (Kigoma, Tanga, Shinyanga, Mwanza, Kilimanjaro, Mbeya, Dodoma, Morogoro na Kagera), na kuendesha mafunzo ya namna ya kuvitumia, kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya UNESCO; na

(l) iliratibu mashindano ya uandishi wa Insha katika nchi

za Jumuiya ya Afrika Mashariki na ya SADC, ambapo wanafunzi wa Tanzania walishika nafasi ya kwanza katika Afrika Mashariki na nafasi ya tatu katika Nchi za Jumuiya ya SADC.

## Idara ya Elimu ya Ualimu

23. **Mheshimiwa Spika**, *Idara ya Elimu ya Ualimu* inasimamia utoaji wa mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada. Aidha, Idara huandaa na kupitia miongozo na viwango vya Elimu ya Ualimu na kufuatilia uendeshaji na utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Ualimu.

24. **Mheshimiwa Spika**, mafunzo ya elimu ya ualimu ngazi ya cheti na Stashahada hutolewa katika vyuo vya ualimu 34 vya Serikali na 69 visivyo vya Serikali vyenye uwezo wa kudahili jumla ya wanachuo 43,098 kwa wakati mmoja.

25. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuinua ubora wa utoaji wa elimu nchini, wizara yangu ilizindua mkakati wa 'Mafunzo ya Walimu Kazini kwa Elimu ya Msingi' - Ngazi ya Shule (MWAKEM) wenye lengo la kuimarisha uwezo wa walimu wa kufundisha pamoja na kuwajengea umahiri katika kufundisha elimu ya awali na msingi. MWAKEM inatimiza lengo la pili la MMEM, ambalo ni kuinua ubora wa elimu kwa kujenga uwezo wa walimu wa shule za msingi ili kuimarisha utoaji wa elimu bora. Utekelezaji wa MWAKEM, unafanyika kwa mfumo wa moduli kwa njia ya elimu masafa. Utaratibu huu unampa mwalimu nafasi ya kujifunza mambo mapya yaliyomo katika mtaala, kupata dhana, nadharia na mbinu bora za kufundishia na kujifunzia ili kukidhi mabadiliko ya kijamii, sayansi na teknolojia, pamoja na kumwezesha mwalimu kujiendeleza kitaaluma na kitaalamu. MWAKEM inatekelezwa

katika ngazi ya shule na hivyo kumwezesha mwalimu kusoma huku akiendelea kufanya kazi. Aidha, kujiendeleza kwa namna hii humwezesha mwalimu kujifunza kwa kutenda awapo shuleni, badala ya kutegemea nadharia za vitabuni. Mafunzo ya namna hii yana gharama ndogo ikilinganishwa na yale ya kukaa chuoni.

26 **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, *Idara ya Elimu ya Ualimu* ilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) ilidahili wanachuo 6,379 wa ngazi ya cheti na 4,189 wa ngazi ya Stashahada katika vyuo vya ualimu vya serikali. Aidha, ilitoa mafunzo kwa walimu 348 katika fani maalumu mbalimbali (k.m. michezo, muziki, sanaa za ufundi na sanaa za maonesho) katika ngazi ya Cheti na Stashahada;

(b) ilitoa wahitimu 11,196 (5,793 wanawake, 5,403 wanaume) wa mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti. Aidha, walimu wanafunzi 7,088 (wanawake 2,410 na wanaume 4,678) walihitimu mafunzo ya ngazi ya Stashahada, ambapo 1,497 ni walimu kazini na 5,591 ni walimu tarajali. Walimu wote wa ngazi ya cheti ni walimu tarajali. Walimu tarajali wa ngazi ya cheti watapangwa kwenda kufundisha shule za msingi na wa ngazi ya stashahada watapangwa kwenda kufundisha shule za sekondari mwezi Julai/Agosti 2011. Walimu kazini watarudi kwenye vituo vyao vya kazi.

(c) iliwezesha wakufunzi 120 kuhudhuria mafunzo ya jinsi ya kutumia TEHAMA katika kufundisha na kujifunza, kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Mafunzo haya yalilenga katika kutekeleza mradi wa TEHAMA katika shule 35 za sekondari na vyuo 7 vya Ualimu kwa majaribio;

(d) iliwezesha utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Masuala Mtambuko na huduma za afya na kinga dhidi ya VVU na UKIMWI kwa wakufunzi 124;

(e) iliendesha mafunzo ya mbinu za Ufundishaji Bainifu na Elimu ya UKIMWI kwa wakufunzi 36, walimu wa shule za Msingi 275, wakaguzi wa shule 12 na waratibu wa vituo vya walimu 9 kutoka katika Wilaya za Mkoa wa Kigoma (Kibondo, Kigoma Vijijini na Kasulu);

(f) iliendesha mafunzo ya ufundishaji wa somo la French kwa wawezeshaji 36 wa shule za sekondari na mafunzo ya jinsi ya kufundisha somo hili katika shule za sekondari kwa walimu 156;

(g) iligharimia mafunzo ya wakufunzi 285 katika vyuo Vikuu mbalimbali ndani na nje ya nchi;

(h) iliwezesha mafunzo kwa wakuu wa vyuo, maafisa na watendaji 74 kuhusu kuinua ubora wa utendaji kazi katika maeneo ya uongozi na uhasibu katika taasisi ya ESAMI;

(i) iliandaa mwongozo wa ufundishaji wa sayansi, english na TEHAMA kwa vitendo katika vyuo vya ualimu;

(j) ilikamilisha moduli za masomo ya hisabati, English, pamoja na ujuzi wa kufundisha kwa umahiri kwa ajili ya programu ya MWAKEM; na

(k) ilitoa mafunzo kwa watendaji wa program ya MWAKEM, 329, walimu mahiri 423, pamoja na kuelimisha walimu 2,052 wa shule za msingi. Aidha, ilitoa mafunzo kwa wawezeshaji 60 wa ngazi za Halmashauri, chuo na shule.

## Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi

27. **Mheshimiwa Spika,** moja ya majukumu ya *Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi* ni kuleta msukumo katika juhudi za Serikali za kukabiliana na ongezeko la watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu. Aidha, idara ina wajibu

wa kutoa fursa ya kujiendeleza kielimu nje ya mfumo rasmi wa shule miongoni mwa vijana na watu wazima, na kusimamia vituo vya magazeti ya elimu katika kanda.

28. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, *Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi* ilitekeleza yafuatayo:
    (a) iliwezesha uandaaji wa vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia vya wanakisomo; vikiwemo Mwongozo wa Mwezeshaji, Kitabu cha Mwanakisomo, Scripts na Filamu za masomo 65 yatakayofundishwa katika mradi wa 'Ndiyo Ninaweza';
    (b) iliratibu uandaaji wa Sera na mwongozo wa 'Elimu Masafa' na 'Ana kwa Ana';
    (c) iliandaa 'Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Elimu juu ya Haki za Binadamu' na 'Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Watu Wazima' – 2011/12 – 2015/16;
    (d) ilifanya ufuatiliaji na tathmini katika wilaya 9 (Ilemela, Dodoma - Manispaa, Songea - Manispaa, Mkuranga, Ngorongoro, Kiteto, Kilindi, Singida - Manispaa na Kigoma (V)) za majaribio ya programu ya 'Ndiyo Ninaweza', ili kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza; na
    (e) ilichapa nakala 100,000 za magazeti ya Elimu katika kanda za kusini na ziwa na kuyasambaza katika wilaya za kanda hizo.

## Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi

29. **Mheshimiwa Spika**, *Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi* ina majukumu ya kubuni, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

30. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2010/11, *Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi,* pamoja na mambo mengine, ilitekeleza majukumu yafuatayo:

(a) iliwezesha kupatikana kwa mtaalam Elekezi wa kuandaa 'Mpango wa Maendeleo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi' (MMEU);

(b) iliwezesha kukutana kwa wahadhiri wa vyuo 12 vya Tanzania na 12 vya Canada katika Warsha mbili zilizofanyika Morogoro chini ya uratibu wa Mradi wa 'Education for Employment ili kuandaa na kuanzisha mitaala inayozingatia umahiri *(Competence-Based)* katika Vyuo vya Ufundi nchini;

(c) ilifanikisha kuwekeana saini hati ya makubaliano *(Memorandum of Understanding)* kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na 'Metsol AB' ya Sweden juu ya kuanzisha mafunzo ya tabia za metali *(Metallurgy)* nchini, ambapo wataalamu kutoka Sweden watakuja nchini kwa ajili ya kuandaa mitaala wakishirikiana na chuo cha Ufundi Arusha.

## Idara ya Elimu ya Juu

31. **Mheshimiwa Spika**, *Idara ya Elimu ya Juu* ina majukumu ya kusimamia na kutathmini sera, sheria, taratibu na miongozo ya utoaji wa Elimu ya Juu. Aidha, Idara ya Elimu ya Juu, kwa kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Mamlaka ya Elimu Tanzania na Vyuo vya Elimu ya Juu, inahakikisha kuwa elimu inayotolewa inazingatia ubora kulingana na mahitaji ya soko la ushindani, na inawafikia walengwa wenye sifa stahiki.

32. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2010/11 Elimu ya Juu ilitolewa katika vyuo vikuu 19 (vya umma 8 na visivyo vya serikali 11 na vyuo vikuu vishiriki 15 (vya Umma 3 na visivyo vya Serikali 12). Kazi za msingi zinazofanywa na Vyuo Vikuu ni kufundisha na kufanya utafiti ambao, pamoja na kuwa sehemu ya taaluma, unalenga katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini miongoni mwa jamii, na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na umma kwa ujumla.

33. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2010/11, *Idara ya Elimu ya Juu* ilitekeleza yafuatayo:

(a) iligharimia mafunzo kwa wanafunzi Madaktari 1,750 wa Binadamu, Meno na Tiba ya Mifugo katika vyuo vya MUHAS, UDOM, HKMU, KCM-College, WBUCHS, IMTU na SUA. Kati ya hao, 84 ni madaktari wa meno na 70 ni madaktari wa tiba ya mifugo;

(b) ilitekeleza utaratibu wa kubadilishana wanafunzi kati ya Tanzania na Msumbiji, na Tanzania na Uganda, ambapo wanafunzi watanzania 68 wanasoma Uganda na 29 wanasoma Msumbiji. Aidha, wanafunzi 50 raia wa Msumbiji na 69 raia wa Uganda wanasoma katika vyuo vikuu nchini Tanzania;

(c) iliwawezesha wanafunzi 5 raia wa China kusomea kozi ya muda mfupi ya lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam chini ya utaratibu wa skolashipu zinazotolewa na Serikali ya Tanzania kwa Serikali ya China katika kutekeleza mkataba wa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya China;

(d) ilifanikisha uelimishaji wa wadau kuhusu fursa za Elimu ya Juu nchini na nje ya nchi pamoja na umuhimu wa uchangiaji wa gharama za Elimu ya juu katika mikoa ya; Rukwa, Kagera, Tabora na Shinyanga. Aidha, uelimishaji

ulifanyika kupitia maonesho ya Taasisi za Elimu ya Juu nchini yaliyofanyika Dar es Salaam tarehe 27-29 Aprili 2011;

(e) ilidhamini mafunzo ya Shahada ya Uzamili na Uzamivu kwa wahadhiri 18 wanaosoma Ujerumani kupitia skolashipu zinazotokana na mkataba kati ya Tanzania na Ujerumani *(DAAD scholarships);*

(f) ilipokea na kuratibu nafasi 132 za masomo; kutoka Uingereza (12), China (72), Korea ya Kusini (2), India (20), New-Zealand (2), Urusi (15), Misri (5) na Cuba (4);

(g) iligharimia mahitaji maalum kwa wanafunzi wenye ulemavu katika vyuo vikuu; UDSM, SUA, MZUMBE, MUCCoBS na DUCE; na

(h) iliratibu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (MMEJU) kwa kukusanya taarifa zinazohusu maeneo ya kipaumbele katika mradi.

## Idara ya Ukaguzi wa Shule

34. **Mheshimiwa Spika**, *Idara ya Ukaguzi wa Shule* ina majukumu ya kuhakikisha kuwa sera, sheria, kanuni na viwango vya utoaji elimu vilivyowekwa vinatekelezwa kwa ufanisi katika ngazi za elimu ya awali, msingi, sekondari, vitengo vya elimu maalum, vituo vya ufundi stadi, Elimu ya Watu Wazima na Elimu nje ya Mfumo Rasmi, na Vyuo vya Ualimu.

35. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2010/11, *Idara ya Ukaguzi wa Shule* ilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) ilikagua Jumla ya asasi za elimu 7,906 na kutoa ushauri na msaada wa kitaalamu na kitaaluma kwa walimu. Aidha, uhaba wa walimu, miundombinu isiyotosheleza, uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vilibainika, katika shule zilizokaguliwa;

(b) iliandaa Mwongozo wa Mafunzo *(Training Manual)* kwa ajili ya wasimamizi wa elimu kwa kushirikiana na UNICEF; na

(c) iliteua wakaguzi 214 na kuwapa mafunzo ya ukaguzi wa shule mwezi Agosti, 2010 na kuwapanga katika Wilaya na kanda husika.

## Idara ya Sera na Mipango

36. **Mheshimiwa Spika**, *Idara ya Sera na Mipango* inahusika na utoaji wa utaalamu na huduma katika uandaaji, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo, pamoja na uratibu wa maandalizi ya Mpango Mkakati wa Muda wa Kati wa Wizara, na Mpango wa Muda wa kati wa Matumizi ya Fedha ya Umma na Mipango ya Utekelezaji wake. .

37. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11 Idara ya Sera na Mipango ilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) iliandaa 'Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo' na kuendelea kuisambaza kwa wadau kwa ajili ya kupata maoni;

(b) iliandaa michoro na miongozo ya ujenzi wa shule za sekondari chini ya MMES Awamu ya Pili (2010-2015);

(c) iliendesha mafunzo kuhusu mipango ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya shule kwa: watendaji 527 wa Halmashauri katika kituo cha ADEM – Bagamoyo, na Maafisa Elimu wa Mikoa na Wakuu wa Shule za Sekondari 924 katika vituo vya ADEM - Bagamoyo, Njombe na Kahama;

(d) iliendelea kusimamia ujenzi wa Shule ya Sekondari ya bweni ya mchepuo wa sayansi kwa ajili ya Kidato cha 5 na 6 Miono - Bagamoyo;

(e) iliendelea kusimamia ujenzi wa shule za Msingi za Msoga (kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China),

(f) iliendelea kusimamia ujenzi wa shule ya Arusha Contonment;

(g) ilifanya tathmini ya hali halisi *(Physical Condition Survey)* ya miundombinu ya vyuo vya ualimu 10 na Maktaba 14 za mikoa ili kubaini mahitaji halisi ya kuifanyia ukarabati;

(h) iliimarisha Mfumo wa Takwimu *(Database)* za elimu katika Halmashauri 105 kwa kushirikiana na UNESCO kupitia programu ya Education Sector Management Information System (ESMIS);

(i) iliendesha Mkutano wa Pamoja wa Mapitio ya Utendaji katika Sekta ya Elimu *(Joint Education Sector Review)* kwa mwaka 2009/10; na

(j) ilifanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Muda wa Kati na kuandaa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2011/12.

## Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu

38. **Mheshimiwa Spika,** *Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu* inasimamia masuala ya utawala, ajira, maslahi na maendeleo ya watumishi pamoja na sheria, kanuni na taratibu za utumishi. Aidha, inaratibu 'Programu ya Kuboresha Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma'.

39. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2010/11, *Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu* ilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) iliratibu ajira za watumishi wapya 351 (walimu 340 na watumishi wasio walimu 11), iliidhinisha vibali vya ajira za watalaam wa kigeni 722, ilithibitisha kazini watumishi 85, na kuratibu upandishaji vyeo wa watumishi 1,010 (walimu 812 na watumishi wasio walimu 198);

(b) ilikamilisha rasimu ya mkataba wa huduma kwa mteja ambapo utekelezaji wake utaanza mwaka wa fedha 2011/12;

(c) Wizara inaendelea kushughulikia madai ya watumishi kila yanapopokelewa. Kati ya Julai 2010 na Juni 2011, Wizara ilihakiki na kuwasilisha Hazina madai mbalimbali ya watumishi 822 yakiwa na thamani ya Sh. 1,269,298,719.60. Kati ya hayo, malimbikizo ya mishahara yalikuwa na thamani ya Sh. 777,918,643.00, na madai mengineyo yalikuwa ya Sh. 491,380,076.60. Aidha, hivi sasa, madai ya watumishi 844, yenye thamani ya Sh. 923,899,277.18 yanashughulikiwa na;

(d) iliandaa mfumo wa kuhifadhi taarifa za watumishi kwa kutumia TEHAMA ambapo taarifa za watumishi zimeanza kuhakikiwa na kuingizwa katika mfumo huo ili ziweze kutumika rasmi mwaka ujao wa fedha 2011/12.

## Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano

40. **Mheshimiwa Spika**, *Kitengo cha Habari*, *Elimu na Mawasiliano* kina majukumu ya kuratibu na kuandaa utoaji wa habari za Sekta ya Elimu kwenye vyombo vya habari na wananchi. Aidha, kinashirikiana na wadau wengine wa sekta ya elimu katika kuhamasisha wananchi katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya elimu.

41. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, Kitengo cha Habari Elimu na Mawasiliano kilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) kiliratibu na kuandaa utoaji wa habari zinazohusu matukio ya elimu yakiwemo, uzinduzi wa MMES Awamu ya II, na mpango wa 'Mafunzo ya Walimu Kazini kwa Walimu wa Shule za Msingi' (MWAKEM);

(b) kilifanikisha kuchapishwa kwa nakala 2,000 za Jarida la EdSDP katika kanda za Elimu na kuzisambaza ili kuhamasisha jamii kuhusu mikakati ya kutekeleza mipango ya elimu;
(c) kiliandaa vipeperushi 500, kalenda 17,500 na shajara 2,000 kwa ajili ya kuwaelezea wadau juu ya sera na mipango mbalimbali ya maendeleo ya Elimu;
(d) kilijibu hoja 30 za wadau kati ya 35 zilizotolewa katika tovuti ya wananchi, (www.wananchi.go.tz), na 5 bado zinafanyiwa kazi; na
(e) kilikamilisha rasimu ya kwanza ya 'Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara'.

## WAKALA, TAASISI NA MABARAZA YA WIZARA

42. **Mheshimiwa Spika,** Wakala, Taasisi na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara yangu yana wajibu wa kusimamia utoaji wa elimu na mafunzo nchini. Mwaka 2010/11, kila Wakala, Baraza na Taasisi zilitekeleza kazi zilizopangwa kwa kuzingatia malengo na mipango ya elimu kama ifuatavyo:

### Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

43. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ina jukumu la kutoa mafunzo ya elimu ya Watu Wazima na elimu ya kujiendeleza nje ya mfumo rasmi nchini.

44. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2010/11, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ilitekeleza mambo yafuatayo:
(a) ilitoa mafunzo ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelezi kwa kutumia mfumo unaozingatia umahiri *(Competence Based Education & Training Curriculum -*

CBET), kwa walengwa 140 wa ngazi ya Cheti, 300 wa Stashahada, 125 wa Stashahada ya juu na 202 wa Shahada;

(b) ilitoa mafunzo ya namna ya kufundisha kwa kutumia mfumo unaozingatia umahiri kwa wakufunzi na wahadhiri 53 wa TEWW na Vyuo 6 vilivyo chini ya NACTE vikiwemo *Tanzania Institute of Accountancy, Institute of Social Work, Tanzania Insurance Institute* na Chuo cha Polisi Moshi na Dar es Salaam;

(c) ilitoa machapisho na majarida ya kitaaluma ya TEWW, Journal of Adult Education No.18, Studies in Adult Education No. 66. na Alumni Newsletter;

(d) ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana tangu ulipoanzishwa 2004-2009 kwa nchi nzima;

(e) ilifanikisha kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaosoma kupitia Mpango wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana kutoka 49,533 mwaka 2009 hadi 62,533 mwaka 2011;

(f) ilizindua utekelezaji wa Programu ya Integrated Post-Primary Education (IPPE) katika wilaya za Siha na Temeke. Masomo ya Ufundi na masuala mtambuko ya programu ya (IPPE) yameandaliwa kwa mtindo wa moduli;

(g) iligharimia mafunzo ya kujiendeleza kwa watumishi 42 katika ngazi zifuatazo: shahada ya uzamivu wahadhiri 2; shahada ya uzamili wakufunzi 5; shahada ya kwanza 2; na mafunzo ya kitaalamu ya muda mfupi kwa watumishi 33 wa kada zisizo za kitaaluma; na

(h) iliandaa na kusambaza nakala 300 za moduli za Elimu Masafa na Ana kwa Ana katika mikoa 15.

## Taasisi ya Elimu Tanzania

45. **Mheshimiwa Spika**, *Taasisi ya Elimu Tanzania* ina majukumu ya kubuni na kuandaa mitaala na mihtasari ya elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu na elimu maalum.

46. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, Taasisi ya Elimu Tanzania ilitekeleza mambo yafuatayo:
    (a) ilitoa mafunzo elekezi kwa walimu 265 wa shule za sekondari;
    (b) iligharimia mafunzo ya waratibu wa mitaala 6;
    (c) ilikamilisha maandalizi ya moduli za masomo 17 kwa ajili ya mafunzo ya ualimu ngazi ya stashahada na cheti na kuzihariri, tayari kwa uchapishaji; na
    (d) iliandaa na kuifanyia majaribio mihtasari 6 ya masomo ya ufundi kwa ajili ya kidato cha 1-4.

## Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania

47. **Mheshimiwa Spika**, *Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania* ina jukumu la kutoa na kusambaza huduma za maktaba nchini; kuanzisha, kuendesha, kuongoza, kuimarisha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma kuanzia ngazi za Vijiji, Wilaya hadi Mikoa, na kutoa mafunzo na kuendesha mitihani ya Taaluma ya Ukutubi.

48. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania ilitekeleza mambo yafuatayo:
    (a) iliwezesha kupatikana kwa jumla ya vitabu 93,914; kati ya hivyo, 817 vilipatikana kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya mwaka 1975, vitabu 87,847 vilipatikana kwa njia ya msaada na vitabu 5,250 vilinunuliwa, na hivyo kufanya

idadi ya vitabu vyote katika maktaba nchini kufikia 1,091,043;

(b) iliwezesha kupatikana kwa machapisho ya magazeti na majarida 32,828. Kati ya hayo, 28,810 ni Magazeti na 4,018 ni Majarida, na hivyo kufanya jumla ya magazeti na majarida yote kufikia 673,730;

(c) ilisambaza jumla ya vitabu 50,670 kwenda katika maktaba 20 za mikoa, 14 za wilaya na 2 za tarafa;

(d) ilitoa ushauri kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa maktaba katika shule 164 na vyuo 60;

(e) iliwezesha udahili wa wanafunzi 579 wa Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka, ambapo wa ngazi ya Cheti walikuwa 264, wa Stashahada 169, na wa mafunzo ya awali 146;

(f) iliwezesha uhitimu wa wanachuo 392 (cheti – 184, Stashahada – 62 na mafunzo ya awali – 146) na

(g) ilikamilisha uandaaji wa michoro ya mabweni mawili ya wanafunzi wa kike, na mkandarasi amepatikana na amekwishaanza kazi ya ujenzi wa bweni la kwanza.

## Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu

49. **Mheshimiwa Spika**, *Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu Bagamoyo (Agency for the Development of Educational Management-ADEM)* una majukumu makuu manne: kuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika uongozi na uendeshaji wa elimu; kutoa ushauri wa kitaalamu katika mambo yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu; kufanya utafiti katika masuala yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu; na kuandaa na kusambaza makala na vitabu mbalimbali vya uongozi na uendeshaji wa elimu.

50. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2010/11, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu ulitekeleza mambo yafuatayo:

(a) ulipanua wigo wa kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa kufungua kituo cha mafunzo kanda ya ziwa kwenye majengo ya kituo cha Taifa cha Kisomo cha Elimu ya Watu Wazima, Mwanza. Kituo kina wanachuo 77; kati ya hao, wanawake ni 43 na wanaume ni 34;

(b) ulitoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa wanachuo 386 kati ya 420 waliotarajiwa. Wanachuo 309 wako kituo cha ADEM-Bagamoyo na 77 wako kituo cha ADEM- Mwanza;

(c) ulitoa mafunzo ya awali ya Ukaguzi wa Shule kwa Wakaguzi wa Shule 214 sawa na asilimia 93.9 ya Wakaguzi 228 waliolengwa;

(d) ulitoa mafunzo ya mwezi mmoja ya uongozi na uendeshaji wa elimu kwa Maafisa Elimu wapya 69 wa ngazi ya Halmashauri, sawa na asilimia 92 ya maafisa 75 waliotarajiwa;

(e) ulitoa mafunzo kwa wakuu wa Shule za Sekondari 881 na Maafisa Elimu 20 wa Mikoa, katika utekelezaji wa MMES Awamu ya II (2010-2015). Washiriki walitoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara;

(f) ulitoa mafunzo juu ya mbinu bora za usimamizi wa shule kwa maafisa 285, ambapo Maafisaelimu wa Mikoa walikuwa 21, Maafisa Elimu wa Elimu ya Sekondari 132 na wa Maafisaelimu wa Elimu ya Msingi 132;

(g) uliandaa mahitaji ya mafunzo kwa ajili ya Kamati za Shule za Msingi, Waratibu Elimu Kata na Bodi za Shule za Sekondari ili kubaini maeneo yatakayopewa kipaumbele katika kuandaa mafunzo. Lengo la mafunzo haya ni kuwawezesha washiriki kusimamia Elimu ya Msingi na Sekondari katika maeneo yao kwa ufanisi;

(h) ulikamilisha 'Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Wakala' *(Master Plan);* na

(i) uligharimia mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi 26 yaliyoendeshwa ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi. Aidha, Wakala ulifadhili mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 6.

## Tume ya Taifa ya UNESCO

51. **Mheshimiwa Spika,** *Tume ya Taifa ya UNESCO* ina majukumu ya kutekeleza programu za UNESCO nchini kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyanja za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni, Mawasiliano na Habari.

52. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/11, Tume ya Taifa ya UNESCO ilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) ilisimamia, kuratibu, pamoja na kutathmini utekelezaji wa miradi ya ushirikishwaji *(Participation Programme)* kulingana na maamuzi ya kikao cha 35 cha Mkutano Mkuu wa Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni *(UNESCO General Conference);*

(b) ilisimamia utekelezaji wa Programu katika sekta tano za UNESCO pamoja na programu ya 'Mwaka wa Kimataifa wa Sayari Dunia' ambapo manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam zilishiriki katika warsha za usafi na utunzaji wa mazingira wa jiji la Dar es Salaam;

(c) iliendelea kusimamia ushiriki wa wataalam wa Tanzania katika programu mbalimbali ikiwemo Programu ya Maji, Programu ya Bahari, Progamu ya Elimu kwa Maendeleo Endelevu na Programu ya Mtu na Mazingira;

(d) ilitoa vitabu na vifaa vya maabara ya lugha kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Zanzibar *(SUZA)*, vitabu, vifaa vya maabara na kompyuta kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Barabara ya Mwinyi, wilayani Temeke na shule ya Umba Korogwe, Tanga, kupitia miradi shirikishi. Aidha, ilisimamia utekelezaji wa mradi wa kuimarisha ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule ya sekondari ya Maneromango - Kisarawe;

(e) iligharimia masomo ya wanachuo 6 wa kike katika ngazi ya uzamili katika masomo ya Sayansi; na kuwezesha uanzishwaji wa Kituo cha Habari kinachotumia TEHAMA kwa ajili ya Baraza la Maendeleo ya Vitabu Tanzania *(BAMVITA);*

(f) iliendelea kushirikiana na wadau katika kuratibu utekelezaji wa 'Programu ya Kuhifadhi Historia ya Ukombozi Barani Afrika' na 'Programu ya Uhuishaji wa Mfumo wa Sayansi,Teknolojia na Ubunifu' kwa kushirikiana na UNESCO. Aidha, ilishirikiana na wadau wa astronomia na kemia katika kutekeleza programu za UNESCO nchini;

(g) ilisimamia mpango wa kuimarisha elimu ya sayansi katika shule zilizo katika mtandao wa UNESCO na kuanza kugawa Vionambali (*Telescope*) 250 katika shule mbalimbali, na kuhamasisha shule nyingi zaidi kujiunga na mtandao wa UNESCO Tanzania Bara na Visiwani;

(h) iliwezesha uwasilishwaji Bungeni Miswada miwili ya Utamaduni kwa ajili ya kuridhiwa: 'Mkataba wa UNESCO wa Mwaka 2001 wa kuhifadhi Urithi wa Kiutamaduni' *(Convention on the safeguarding of Intangible Cultural Heritage)* na 'Mkataba wa UNESCO wa 2005' - Convention on the Protection and Promotion of Cultural Diversity Expressions, kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijana na Michezo;

(i) iliratibu ushiriki wa Tanzania katika kikao cha 34 cha Kamati ya Kimataifa ya Urithi wa Dunia, kilichofanyika nchini Brazil tarehe 25 Julai – 3 Agosti 2010, kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii;

(j) ilitekeleza mpango wa pamoja wa mafunzo kwa watendaji wake na kuendesha warsha za kuwajengea uwezo watumishi wa Tume husika kwa kushirikina na Tume za Taifa za UNESCO za Afrika ya Mashariki;

(k) iliratibu mchakato wa uteuzi wa awali wa vijana 12 watakaoshiriki katika ushindani wa nafasi za kazi za UNESCO *(Young Professionals Programme)*; na

(l) ilichapisha na kusambaza toleo Na. 7 la jarida la 'Tanzania na UNESCO'.

## Baraza la Mitihani la Tanzania

53. **Mheshimiwa Spika**, *Baraza la Mitihani la Tanzania* lina jukumu la kutekeleza sera ya mitihani kwa kuzingatia Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha, Baraza lina jukumu la kuendesha Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi na Sekondari, Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada, mtihani wa Maarifa, na kusimamia uendeshaji wa mitihani itolewayo na bodi za nje ya nchi.

54. **Mheshimiwa Spika,**, katika mwaka 2010/11, Baraza la Mitihani la Tanzania lilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) liliendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2010 kwa watahiniwa 895,013;

(b) liliendesha Mitihani ya: Kidato cha Nne ya mwaka 2010, Maarifa (QT) wa mwaka 2010, Kidato cha Sita 2011 na Ualimu 2011 kwa jumla ya watahiniwa 543,805;

(c) lilisimamia Mitihani inayotolewa na Bodi za Nje ya nchi kwa watahiniwa 65;

(d) lilinunua *server* tatu zenye uwezo mkubwa kwa ajili ya matumizi yafuatayo:
- kusajili watahiniwa kupitia mtandao *(online)*,
- kuchambua mitihani ya Taifa pamoja na kuhifadhi taarifa za matokeo na picha za watahiniwa waliofanya mtihani,
- kusanifu na kukuza mifumo inayotumika katika Baraza la Mitihani;

(e) lilikamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitano 2010/11 - 2015/16; na

(f) lilikamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa kituo cha usahihishaji cha Mbezi Wani.

## Kituo cha Maendeleo Dakawa

55. **Mheshimiwa Spika,** *Kituo cha Maendeleo Dakawa* kina majukumu ya kutunza na kuhifadhi majengo, vifaa na miundombinu iliyokabidhiwa na ANC kwa ajili ya kulinda Historia ya Ukombozi wa Kusini mwa Afrika. Baada ya Serikali ya Tanzania kukabidhiwa Kituo cha Maendeleo Dakawa kutoka kwa Wapigania Uhuru wa ANC, Wizara yangu imekusudia kukiendeleza kituo hiki na kukitumia katika kutoa Elimu ya Sayansi na Ufundi kupitia taasisi zilizopo na zitakazoainishwa hapo baadaye ili kiwe kitovu cha utoaji wa elimu *(Centre of Excellence)*.

56. **Mheshimiwa Spika,** Kituo cha Maendeleo Dakawa chenye eneo la ekari 7,500, kina jumla ya nyumba 82 za kuishi watumishi na majengo mengine muhimu yanayowezesha uendeshaji wa mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada kwa wanachuo 783. Aidha, kituo kina shule ya sekondari ya juu ya wasichana ya kidato cha 5 na 6 (Shule ya Sekondari Dakawa) yenye wanafunzi 450 na wafanyakazi 26; Chuo cha Ufundi Stadi – VETA chenye

wanachuo 160 na Wafanyakazi 20; Shule ya Msingi yenye walimu 15, wanafunzi 400 wa elimu ya msingi na 50 wa Elimu ya Awali. Aidha, kuna Zahanati inayotoa huduma kwa wanajamii waliopo ndani na nje ya Kituo. Zahanati hii ina Maafisa Tabibu wawili na Wauguzi watatu.

## Mamlaka ya Elimu Tanzania

57. **Mheshimiwa Spika**, *Mamlaka ya Elimu Tanzania* ina majukumu ya kutafuta na kubaini vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kugharimia maendeleo ya sekta ya elimu nchini ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wadau wa elimu kuchangia kwa hiari katika miradi ya elimu.

58. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, Mamlaka ya Elimu Tanzania ilitekeleza mambo yafuatayo:
    (a) iliendesha harambee kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi 2,298 wenye ulemavu katika shule 49 kwa kuwapatia vifaa vya kujifunzia na visaidizi; ambapo kiasi cha Sh. Milioni 491.2 zilipatikana.
    (b) iliimarisha miundombinu ya shule 116 za msingi na sekondari, na vyuo vya elimu ya juu 8, kwa kufadhili miradi ya maboresho ya jumla ya Sh. bilioni 2.1 kutoka kwenye Mfuko wa Elimu;
    (c) ilifanya ufuatiliaji, ukaguzi na tathmini katika miradi 120 iliyofadhiliwa na Mfuko wa Elimu;
    (d) iliendelea kuhamasisha Halmashauri za Serikali za Mitaa kuanzisha Mifuko ya Elimu na kuimarisha ushirikiano na 'Jumuiya ya Serikali za Mitaa Tanzania'. Aidha, ilihamasisha uchangiaji wa mfuko wa elimu kupitia vipindi vya televisheni na redio, vipeperushi, majarida na vyombo vingine vya habari; na

(e) ilikamilisha andiko la marekebisho la vyanzo vya mapato ya mfuko ikiwa ni hatua ya mchakato wa marekebisho ya Sheria ya mfuko wa Elimu ya mwaka 2001.

## Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania

59. **Mheshimiwa Spika**, *Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania* ina majukumu ya kutoa ithibati, kuratibu uanzishwaji wa Vyuo Vikuu, kusimamia ubora wa elimu na kuidhinisha programu zinazofundishwa, ili zikidhi mahitaji ya Taifa na soko la ajira.

60. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) ilitathmini ubora wa programu 140 za masomo ya vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki nchini;

(b) iliandaa na kuendesha warsha na semina 12 za mafunzo ya uelimishaji umma kuhusu majukumu ya Tume na mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi wa vyuo vikuu nchini;

(c) ilikamilisha rasimu ya kwanza ya mfumo wa tuzo zinazotambuliwa kitaifa *(National Qualifications Framework)* na maandalizi ya kanuni zake;

(d) ilitathmini na kutambua vyeti 300 vilivyowasilishwa na wahitimu wa vyuo vikuu vya nje ya nchi;

(e) iliratibu na kutathmini mradi wa majaribio ya udhibiti wa ubora wa programu za vyuo vikuu 5 vinavyotekeleza mradi chini ya *Inter-University Council for East Africa* (IUCEA);

(f) ilichapisha na kusambaza nakala 20,000 za kitabu cha Mwongozo wa mwanafunzi, nakala 1,000 za vitabu vyenye taarifa fupi za vyuo vikuu nchini, na vipeperushi mbalimbali vinavyomwelekeza mwanafunzi jinsi ya kuomba kudahiliwa katika vyuo vya elimu ya juu nchini. Aidha, Tume ilitoa taarifa mbalimbali zinazoelimisha umma juu ya majukumu ya Tume;

(g) ilikagua na kutathmini mipango ya kuanzisha au kuhuisha vyuo vikuu 8 (Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan - Morogoro, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi ya Afya cha Mtakatifu Fransis - Ifakara Morogoro, Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mihayo - Tabora, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sebastian Kolowa - Lushoto, Tanga, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Bugando - Mwanza, Chuo Kikuu cha Bagamoyo, Chuo Kikuu kishiriki cha Bukoba, na Kitivo cha Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino-Mtwara), kwa lengo la kutoa hati husika;

(h) iliratibu na kusimamia udahili wa wanafunzi 533,195 kwa kutumia mfumo mpya wa udahili wa wanafunzi wa vyuo vya Elimu ya juu ujulikanao kama *Centralized Admission System* (CAS). Mfumo huu unahusisha vyuo 53 vya Elimu ya juu vikiwemo vyote vya umma na baadhi vya binafsi;

(i) iliratibu maonesho ya sita ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yaliyofanyika Dar-es Salaam tarehe 27-29 Aprili 2011 ambayo kauli mbiu yake ilikuwa *Building a Knowledgeable, Responsible, Accountable and Progressive Society, through Higher Education Science and Technology.* Aidha, jumla ya taasisi na asasi 62 zilishiriki kutoka ndani na nje ya nchi, nyingi zikiwa ni vyuo vya elimu ya juu; na

(j) iliendesha mafunzo ya kuwaelimisha watumishi wake wote juu ya Sheria mpya ya kupambana na kuzuia rushwa nchini. Aidha watumishi wote walishiriki kwenye mafunzo ya siku mbili juu ya tathmini ya ndani ya majukumu ya tume, kwa lengo la kuinua ubora wa utendaji wa tume na kuhimiza uwajibikaji.

## Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi

61. **Mheshimiwa Spika,** *Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi* lina majukumu ya kusimamia na kuratibu mitaala, ubora wa mafunzo, mitihani, tuzo, usajili na ithibati za vyuo vya elimu ya ufundi vya umma na binafsi nchini.

62. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2010/11, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi lilitekeleza mambo yafuatayo:
   (a) lilikagua na kutoa idhibati kwa vyuo 20 na kusajili vyuo 20;
   (b) lilibaini na kusajili walimu 400 katika Vyuo vya Ufundi;
   (c) liliratibu mitihani katika vyuo 30;
   (d) lilisimamia uandaaji wa mfumo wa kudhibiti na kuhakiki ubora wa mafunzo katika vyuo 20;
   (e) liliratibu udahili wa wanafunzi wa shahada na stashahada katika vyuo 17;
   (f) liliratibu na kudhibiti utekelezaji wa masharti ya ithibati katika vyuo 20; na
   (g) liliendesha mafunzo katika vyuo 20 juu ya kufundisha kwa kutumia mitaala mipya ya mafunzo ya walimu wa ufundi.

## Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

63. **Mheshimiwa Spika,** *Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu* ina majukumu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi raia wa Tanzania wanaosoma katika Taasisi za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi na kukusanya marejesho ya mikopo hiyo.

64. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2010/11, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilitekeleza mambo yafuatayo:
   (a) ilitoa mikopo kwa wanafunzi 91,568 wakiwemo 23,141

wanaochukua masomo ya sayansi. Aidha, ilifanikiwa kukusanya marejesho ya mikopo yenye thamani ya Sh. 7,998,848,817.87 kati ya Sh. bilioni 21 zilizofikia muda wake wa kukusanywa.

(b) ilihamasisha ukusanyaji wa marejesho ya mikopo kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu wajibu wa kila mdau katika urejeshaji wa mikopo kwa njia mbalimbali, zikiwemo za warsha, mikutano, vipeperushi, magazeti, redio na televisheni. Aidha, Bodi ilikamilisha kutengeneza Hifadhi Data (database) ya wakopeshwaji wote kuanzia mwaka 1994 hadi Juni, 2010; na

(c) ilianza kutumia mfumo wa kupokea maombi ya mikopo kwa njia ya mtandao ujulikanao kama *Online Application System* (OLAS) ambapo waombaji hujaza na kutuma taarifa zao moja kwa moja kwenye Bodi na hivyo kurahisisha zoezi zima.

## Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

65. **Mheshimiwa Spika**, *Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)* ina majukumu ya kuratibu, kudhibiti, kugharimia, kutoa na kukuza elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.

66. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2010/11, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) ilikamilisha upembuzi yakinifu wa ukarabati wa vyuo vya ufundi stadi vya Wilaya za Karagwe na Korogwe pamoja na kuandaa michoro ya majengo na pia kufanya makubaliano *(Memorandum of Understanding - MOU)* kati yake na Halmashauri za Wilaya husika. Kazi ya ukarabati wa vyuo imepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2011/12;

(b) ilidhamini mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wake 513 katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo wa kazi. Kati ya watumishi hao, 269 ni wakufunzi na 244 ni watumishi wa waendeshaji;

(c) ilifanya ukarabati wa vituo viwili vya Ufundi Stadi vya Mwanza na Kihonda, pamoja na kununua na kufunga mashine za kisasa katika karakana ya mafunzo ya Chuo cha Ufundi Stadi cha Dar es Salaam;

(d) ilikamilisha utafiti katiti *(Tracer Study)* kwa nchi nzima ili kufahamu hali ya ajira ya Wahitimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi, ambapo sampuli ya Wahitimu 4,923 wa mwaka 2004 hadi 2009 walifuatiliwa;

(e) iliendeleza ujenzi wa vituo vya mafunzo ya ufundi stadi vya Lindi, Manyara, Pwani, Makete na Kituo cha Mafunzo ya TEHAMA kinachojengwa Kipawa jijini Dar es Salaam;

(f) ilikamilisha ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Hoteli na Utalii huko Njiro – Arusha ili kuanza mafunzo rasmi katika mwaka wa fedha 2011/12;

(g) ilitoa mafunzo katika ngazi ya Stashahada kwa Walimu 32 katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi - Morogoro. Walimu wengine 95 walipatiwa mafunzo ya ngazi ya Stashahada ya Ualimu wa Ufundi katika Chuo hicho. Aidha, jumla ya Walimu wa Ufundi Stadi 60 kutoka Tanzania Visiwani walipatiwa mafunzo ya 'Ufundishaji Unaozingatia Umahiri' *(Competence Based Education and Training)*. Walimu wengine 21 wa ufundi stadi walipewa mafunzo ya ufundishaji wa elimu ya ujasiriamali yaani *Master Trainers for Micro Enterprises*. Vilevile, walimu 50 wa ufundi stadi walipatiwa mafunzo ya ushauri wa kazi za kufanya baada ya kumaliza masomo *(Career Guidance and Counselling for Vocational Training Teachers);* na

(h) ilianzisha na kutekeleza mpango wa mafunzo ya ufundi viwandani uitwao *Skills Enhancement Programme (SEP)* na zoezi hili lilianza na majaribio *(Pilotting)* ya makampuni 7. Chini ya mpango huo, wafanyakazi 235 wamepatiwa mafunzo ya kukuza ujuzi wa kazi. Wafanyakazi hao ni kutoka makampuni na viwanda vya: Saruji - Tanga, Tumbaku - Morogoro, Mabati *(Aluminium Africa - ALAF)* - Dar es Salaam, Chemi Cotex, TPC - Moshi na Hoteli ya Movenpick.

## Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

67. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu.

68. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2010/11, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitekeleza mambo yafuatayo:

a) kilidahili jumla ya wanafunzi 7,024; kati yao 5,029 ni wa shahada ya kwanza (wanawake 1,813, wanaume 3,216). Wanafunzi wa shahada za uzamili na uzamivu walikuwa 1,995 *(wanawake 571, wanaume 1,425);*

b) kiliendeleza ushirikiano na wafadhili mbalimbali katika kugharimia shughuli za taaluma na utafiti, na kusambaza matokeo yake kwa wadau mbalimbali;

c) kilitoa machapisho ya vitabu 25 na majarida 290 na kusambaza matokeo ya utafiti katika nyanja mbali mbali kama za mazingira, ujasiriamali, nishati, utalii, sekta isiyo rasmi, TEHAMA, sayansi asilia na timizi *(Natural and Applied Sciences)*, uhandisi, mabadiliko ya tabianchi, miundombinu, lugha, utawala bora na demokrasia;

d) kiliandaa utaratibu mpya wa ujenzi wa makao makuu mapya ya Taasisi ya Sayansi za Bahari eneo la Buyu,

Zanzibar; ambapo ujenzi huo sasa utafanyika kwa awamu tano, kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha;

e) kiliendeleza ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya chuo kama vile mabweni ya wanafunzi, madarasa, maabara, barabara, mabomba ya maji safi na majitaka, ili kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

f) kilianzisha shahada za kwanza mbili mpya *(B.A. in Kiswahili na B.Sc. in Actuarial Sciences)*, shahada mpya tatu za uzamili *(Master's in Intergrated Sanitation Management, MSc. in Biodiversity and Conservation na Master's in International Trade)* na shahada mpya moja ya uzamivu (PhD. by Coursework and Dissertation in Political Science and Public Administration);

g) kilifanya ukaguzi wa kitaaluma, menejimenti na uendeshaji katika Vyuo vyake, Shule Kuu, Taasisi na Idara zote kwa lengo la kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa na ufanisi wa shughuli zake. Ukaguzi ulifanywa na Kamati Teule ya Mkuu wa Chuo *(Chancellor's Visitation Team*);

h) kilianzisha mchakato wa maandalizi ya shahada mpya nne za uzamivu *(PhD. by coursework and dissertation)* katika Taasisi ya Taaluma za Maendeleo, Idara ya Sayansi za Bahari, Idara ya Zoologia na Fani ya Sayansi za Jamii;

i) kilianza mchakato wa kusherehekea miaka 50 ya Chuo tangu kilipoanzishwa mwezi Oktoba 1961, kwa kuandaa shughuli mbalimbali kama midahalo, makongamano, na semina; na

j) kilianza mchakato wa kujenga 'Kituo cha Wanafunzi' yaani *(UDSM Students Centre*) ikiwa ndiyo azma ya Chuo katika kusherehekea miaka 50. Juhudi za uchangishaji na kutafuta fedha zilianza pia.

## Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam)

69. **Mheshimiwa Spika**, *Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam* ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo hiki kina majukumu ya kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Elimu na Ualimu.

70. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, *Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam* kilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) kilidahili wanachuo wapya 150 wa masomo ya sayansi na 1,007 wa masomo ya Sanaa na Sayansi za Jamii, na kufanya jumla ya wanachuo wapya waliodahiliwa chuoni hapo kuwa 1,157. Ukiongeza idadi ya wanachuo 946 wa mwaka wa pili na 763 wa mwaka wa tatu, jumla ya wanachuo wote ni 2,866;

(b) kilinunua kemikali za maabara zenye thamani ya shilingi 25,706,100.- kwa ajili ya kufanyia mazoezi kwa vitendo; na

(c) kiliendelea kushirikiana na vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hususan kwa shahada za uzamili na uzamivu, ambapo jumla ya wahadhiri 42 wako kwenye mafunzo ya shahada za uzamili, 2 kwenye stashahada na 54 kwenye shahada za uzamivu ndani na nje ya nchi. Mhadhiri mmoja alimaliza shahada ya uzamivu mwezi Januari, 2011 na kurudi chuoni kuendelea na kazi.

## Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam)

71. **Mheshimiwa Spika**, *Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa* ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo hiki kina majukumu ya kufundisha, kutafiti, na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Elimu na Ualimu.

72. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kilitekeleza mambo yafuatayo:
    (a) kiliongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza kutoka 880 hadi 950.
    (b) kilianza ujenzi wa ukumbi wa mihadhara;
    (c) kiliendelea kuimarisha na kupanua miundombinu ya kusomea na kujifunzia; na
    (d) kiliendelea kugharimia masomo ya wahadhiri 68 katika viwango vya uzamili na uzamivu.

## Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo

73. **Mheshimiwa Spika**, *Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo* kinatekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo ya Shahada za Kwanza, Shahada za Uzamili na Uzamivu; na kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za Kilimo, Misitu, Mifugo, Mazingira, wanyama pori, ufugaji wa samaki na fani nyingine za Sayansi na Teknolojia.

74. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilitekeleza mambo yafuatayo:
    (a) kiliendeleza utafiti unaolenga katika kuinua ubora wa kilimo, hifadhi za misitu, mifugo na maliasili nyingine, ikiwa ni pamoja na matumizi ya wanyamakazi katika Kilimo

sehemu mbalimbali nchini, (Kisilo wilaya ya Njombe); Mradi wa mbinu bora za ufugaji wa kuku wa kienyeji (katika Wilaya za Morogoro Mjini na Vijijini, na Mvomero); ambapo wakulima zaidi ya 1,300 hufaidika kila mwaka;

(b) kiliendeleza hifadhi na ukarabati wa Chanzo cha Maji cha mto Mzinga kwa kushirikiana na jamii;

(c) kiliendelea kutoa elimu kwa wanavijiji juu ya umuhimu wa upandaji miti, ufugaji nyuki na kuongeza matumizi ya pembejeo na ukuzaji wa soko kwa aina za miti isiyojulikana na isiyotumika sana nchini Tanzania, chini ya mradi wa *Programme for Agricultural and Natural Resources Transformation for Improved Livelihood* (PANTIL). Aidha, kilihamasisha Mikoa ya Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Arusha kupanda na kutumia miti hiyo. Vilevile, mradi huu ulitoa makala 11 kwenye majarida ya kisayansi;

(d) kilitoa ushauri wa kitaalamu katika kilimo, mifugo, misitu, wanyamapori, umwagiliaji na tiba ya wanyama;

(e) kiliendelea na mradi wa 'Uboreshaji wa Zao la Maharage' ambao umewezesha kutoa aina za maharage za 'Pesa' na 'Mshindi' ambazo hupevuka mapema na kuiva haraka wakati wa kupika; na

(f) kilianzisha shahada mpya 6 za kwanza ambazo ni: *Bachelor of Science in Human Nutrition; Bachelor of Science in Family and Consumer Sciences; Bachelor of Irrigation and Water Resources; Bachelor of Bioprocess and Post-harvest Engineering; Bachelor in Applied Agricultural Extension na Bachelor of Agricultural Education* zilizodahili jumla ya wanafunzi 470 katika mwaka wa masomo 2010/11. Aidha, Chuo kilianzisha stashahada 2 za Maktaba ambazo ni: *Diploma in Records, Archives and Management na Diploma in Library Information Science* na stashahada nyingine 2 za

*Diploma in Tropical Animal Health na Diploma in Laboratory Technology Science zitakazoanza 2011/12.*

## Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Elimu ya Biashara cha Moshi
## (Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo)

75. **Mheshimiwa Spika**, *Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Elimu ya Biashara* ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Chuo kina majukumu ya kufundisha, kufanya utafiti na kutoa ushauri katika nyanja za ushirika, maendeleo ya jamii, biashara, oganaizesheni, ujasiriamali na masuala mtambuko.

76. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11 *Chuo Kishiriki cha Ushirika na Elimu ya Biashara Moshi* kilitekeleza mambo yafuatayo:
    (a) kilidahili jumla ya wanafunzi 3,775 (wa kike 1,469), ambapo udahili wa wanafunzi wa kike uliongezeka kutoka 980 mwaka 2009/10 hadi 1,469 mwaka 2010/11. Hili ni ongezeko la asilimia 49.9. Aidha, ongezeko hili linatokana na kuanzishwa kwa kozi za cheti katika Kampasi ya Kizumbi (Shinyanga) na programu mpya katika Kampasi ya Moshi.
    (b) kiliwezesha jumla ya Wahadhiri 31 kwenda masomoni kwa ajili ya shahada za uzamili (16) na uzamivu (15);
    (c) kiliimarisha matawi manne ya kanda huko Mtwara, Iringa, Mwanza na Tanga na kuyafanya yajikite zaidi katika kutoa elimu kwa jamii katika masuala ya vyama vya ushirika vya akiba na mikopo (SACCOS), utunzaji wa mazingira na mikakati ya kupunguza umaskini;
    (d) kiliendelea na ukarabati wa miundombinu na kufanikiwa kufanya yafuatayo:
        - kuongeza ghorofa moja kwa ajili ya ofisi kwenye

Jengo la Utawala *(Block B),* ambapo ofisi 18 na ukumbi wa mikutano vimeweza kuongezwa;
- kuunganisha 'Jengo la Kilimanjaro' na 'PPP' ili kupata ofisi kwa ajili ya Taasisi ya Maendeleo Endelevu ya Ushirika na Elimu;
- kukarabati baadhi ya nyumba za wafanyakazi na vyumba vya semina na kumbi za mihadhara;
- kutengeneza barabara za ndani katika kampasi ya Kizumbi-Shinyanga kwa kushirikiana na VETA Shinyanga na kukarabati majengo na zahanati;
- kukarabati barabara za ndani na mifereji ya maji ya mvua kuzunguka eneo la utawala na madarasa katika kampasi ya Moshi;

(e) kilifanya upanuzi wa zahanati ya Chuo katika kampasi ya Moshi, ambapo jumla ya vyumba sita vimeongezwa, vikiwemo wodi ya akina mama, ofisi tatu, chumba cha kliniki na chumba cha dawa; na

(f) kilifanya utafiti katika maeneo ya:
- *Role of Cooperative in Regional Economy*
- *SACCOS' Loan Recovery in Cooperative Development in Tanga*
- *Role of Produce Marketing Groups in Poverty Alleviation*
- *Improving Crop Markets and Marketing Information System of Oil Seed Crops: The Case of Groundnuts in Dodoma Region.*

## Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

77. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo Kikuu Huria cha Tanzania* kina majukumu ya kutoa Elimu ya Juu kwa njia ya Masafa na Ana kwa Ana, kutafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na kueneza maarifa kupitia vituo vyake vilivyopo mikoani.

78. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, *Chuo Kikuu Huria cha Tanzania* kilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) kilidahili wanafunzi wapya 8,973 wa cheti, stashahada na shahada (wanawake 3,209 na wanaume 5,764) katika ngazi mbalimbali ambapo, wanafunzi wa vyeti na stashahada walikuwa 3,145, wa shahada ya kwanza 3,749 na wa stashahada na shahada za uzamili na za uzamivu 2,079;

(b) kilifanikisha kuhitimu kwa jumla ya wanafunzi 2,373 (wanawake 956). Kati ya hao, wahitimu wa stashahada, shahada za uzamili na uzamivu walikuwa 167 (wanawake 41);

(c) kilifanya ukarabati wa majengo ya vituo vya mikoa ya Kagera, Rukwa, Kilimanjaro, Ruvuma na Mara. Aidha, kilifanya ukarabati katika vituo vya mikoa tarajiwa ya Njombe na Katavi;

(d) kilifanikisha kupatikana kwa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa vituo na ununuzi wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za vituo katika Mikoa ya Lindi (ekari 100), Mwanza (ekari 17), Kigoma (ekari 22), Shinyanga (ekari 68), Pemba (ekari 4) Pwani (ekari 2), Manyara (ekari 24), Dodoma (ekari 2) na Tabora (ekari 100); na

(e) kilinunua kiwanja kilicho karibu na majengo ya Chuo huko Mbeya ili kujenga hoteli kwa makubaliano maalum na wawekezaji.

## Chuo Kikuu Ardhi

79. **Mheshimiwa Spika**, *Chuo Kikuu Ardhi* kina majukumu ya kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika nyanja mbalimbali zikiwemo za maeneo ya ardhi, nyumba, mazingira na ujenzi.

80. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2010/11, Chuo Kikuu Ardhi kilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) kilidahili wanafunzi wapya 1,013 wa shahada ya kwanza, wanafunzi 64 wa shahada za uzamili na uzamivu, na 19 wa ngazi ya cheti. Jumla ya wanafunzi wote chuoni ni 2,806. Hili ni ongezeko la asilimia 31 ikilinganishwa na mwaka wa masomo 2009/10 ambapo chuo kilikuwa na jumla ya wanafunzi 2,143. Aidha, idadi ya wanafunzi wa kike pia imeongezeka kutoka wanafunzi 634 mwaka 2009/10 hadi 744 mwaka 2010/11, ikiwa ni ongezeko la asilimia 17.3. Idadi ya wanafunzi wa kike ni asilimia 26.5 ya wanafunzi wote waliopo chuoni. Hili ni ongezeko la takriban asilimia tatu ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Mwaka wa masomo 2009/10 wanafunzi wa kike walikuwa asilimia 24 ya wanafunzi wote;

(b) kilianzisha programu mpya mbili (2) za shahada ya kwanza ambazo ni Uhandisi Ujenzi *(Civil Engineering)* pamoja na Fedha na Uhasibu *(Finance and Accounting);*

(c) kiligharimia mafunzo ya wanataaluma wapya 13 na wafanyakazi waendeshaji wapya 12;

(d) kilikamilisha awamu ya 4 ya ujenzi wa jengo jipya la mihadhara na ofisi *(Lands Building),* na hivyo kuweza kupata madarasa 17 ya ziada yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,580 kwa wakati mmoja. Kukamilika kwa jengo hili pia kumewezesha upatikanaji wa nafasi za bohari kwa ajili ya programu ya uhandisi ujenzi na karakana ya Skuli ya Jiomatiki;

(e) kilikamilisha kazi ya kutengeneza mfumo wa usambazaji wa maji safi kwenye mabweni kwa kuongeza matanki. Aidha ilifanya ukarabati wa miundombinu ya majengo ya vyoo, ofisi, madarasa na mabweni, na kuongeza vitanda; na kukamilisha ukarabati wa mfumo wa majitaka kwenye

mabweni yote na ujenzi wa mtambo wa kuchuja majitaka. Zaidi ya hayo chuo kilifanikiwa kujenga mabenchi 70 ya zege kwenye maeneo ya mabweni na madarasa kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi;

(f) kiliandaa michoro ya awali ya jengo jipya la kumbi za mihadhara na ofisi za wahadhiri pamoja na ya makazi ya Makamu Mkuu wa Chuo na mabweni ya wanafunzi; na

(g) kilikamilisha maandalizi ya maandiko manane (8) ya miongozo na taratibu za uendeshaji wa Chuo.

## Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili

81. **Mheshimiwa Spika**, *Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili* kina majukumu ya kufundisha, kutafiti, kutibu na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya tiba na afya.

82. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2010/11 *Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi* Shirikishi Muhimbili kilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) kilidahili wanafunzi 342 wa shahada ya kwanza katika fani mbalimbali za afya na tiba, na wanafunzi 218 katika shahada za uzamili na uzamivu;

(b) kilifanikiwa kumpata mshauri elekezi wa kuandaa Master Plan pamoja na makisio ya gharama za ujenzi wa hospitali katika kampasi ya Mloganzila ambapo kazi imeanza;

(c) kilifanikiwa kukamilisha taratibu zote za makubaliano ya mkopo nafuu kutoka Serikali ya Korea ya Kusini na kusaini mkataba wa mkopo huo tarehe 15/09/2010, ambapo mshauri elekezi wa ujenzi wa hospitali katika kampasi ya Mloganzila amepatikana na kuanza kutengeneza michoro *(hospital design)*;

(d) kilifanya ukarabati wa: mgahawa wa wanafunzi katika kampasi ya Muhimbili, kumbi za mihadhara ya kufundishia

katika kampasi za Muhimbili na Bagamoyo, na baadhi ya nyumba za wafanyakazi zilizoko Bagamoyo;

(e) kiliweka samani katika mgahawa mpya wa wanafunzi uliopo Barabara ya Chole Dar es Salaam na miundombinu ya mawasiliano katika jengo jipya la kampasi ya Muhimbili;

(f) kilikalimisha utafiti wa awali kuhusu upatikanaji wa kipimo cha kugundua ugonjwa wa malaria kwa haraka *(rapid diagnostic colour test)* na kuwasilisha taarifa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii;

(g) kilikamilisha utafiti wa 'Chanjo ya Majaribio dhidi ya UKIMWI' *(Clinical Trial of HIV Vaccine)* ambapo matokeo ya awali yanaonyesha kuwa chanjo hii ni salama na hivyo ina uwezo wa kuufanya mwili kutengeneza vichocheo vya kinga dhidi ya Virusi vya UKIMWI. Hata hivyo, bado haijathibitika iwapo chanjo hiyo ina uwezo wa kukinga watu wasipate maambukizi mapya ya VVU au kupunguza ongezeko la virusi vya UKIMWI mwilini; na

(h) kiliendelea kufanya utafiti wa aina mbalimbali za magonjwa ya akina mama na watoto katika maeneo yafuatayo:

- namna ya kupunguza vifo vya watoto wachanga *(perinatal mortality)*,
- uboreshaji wa huduma ya wajawazito na wazazi hususan rufaa wakati wa dharura;
- matukio ya kubakwa na kudhalilishwa watoto, na
- unyanyasaji wa kijinsia ikijumuisha ubakaji na ukatili majumbani.

## Chuo Kikuu Mzumbe

83. **Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu Mzumbe kina majukumu ya kutafuta, kukuza, kuhifadhi na kueneza maarifa na stadi za menejimenti kwa njia ya mafunzo, utafiti na huduma za kiufundi na kitaalamu.

84. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2010/11, Chuo Kikuu Mzumbe kilitekeleza mambo yafuatayo:
    (a) kilidahili jumla wa wanafunzi 3,545 ambapo, 1,283 walikuwa wa Shahada ya Kwanza (623 wa kike), 92 stashahada (44 wa kike), 277 cheti (110 wa kike) na 1,943 wa shahada za uzamili (777 wa kike);
    (b) kiliwezesha wahadhiri 11 kujiunga na masomo ya shahada ya uzamivu na wengine 19 katika shahada ya uzamili. Aidha, wahadhiri saba walirudi kazini baada ya kuhitimu shahada za uzamivu na wengine 12 shahada za uzamili. Wahadhiri wengine 62 wanaendelea na masomo ya uzamivu na 12 uzamili;
    (c) kilikamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa kike yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200. Aidha, awamu ya pili ya ujenzi inayoendelea itaiwezesha hosteli kuchukua wanafunzi wengine 200, ambapo mkandarasi anakamilisha ujenzi wa kuta katika ghorofa ya nne;
    (d) kilikamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa tatu la ofisi za wahadhiri na kuziwekea samani;
    (e) kiliwezesha ujenzi wa kuta za maktaba kufikia kimo cha kuanza kuweka madirisha. Maktaba hiyo ikikamilika, itakuwa na uwezo wa kuchukua wasomaji 600 kwa wakati mmoja; na
    (f) kilikamilisha upatikanaji wa vitalu vitatu vilivyopo Upanga ambapo taratibu za kuhamisha miliki za viwanja hivyo kutoka NHC kwenda Chuo Kikuu Mzumbe zinaendelea.

## Chuo Kikuu cha Dodoma

85. **Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu cha Dodoma kina majukumu ya kutoa mafunzo ya Shahada za Kwanza na za Juu, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika nyanja za Ualimu, Hisabati, Sanaa na Lugha, Sayansi za Jamii, Tiba na Uuguzi, Sayansi za Kompyuta, na Sayansi Asili.

86. **Mheshimiwa Spika**,, katika mwaka 2010/11 *Chuo Kikuu cha Dodoma* kilitekeleza mambo yafuatayo:
   (a) kilidahili wanafunzi wapya 8,000. Aidha, kilidahili wanafunzi 600 wa shahada za uzamili;
   (b) kilikamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa Chuo cha Sanaa za Lugha na Sayansi za Jamii, na kukifanya chuo hicho kuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 20,000;
   (c) kilikamilisha ujenzi wa barabara za ndani kwa asilimia 80%. Aidha, miundombinu ya maji-safi na maji-taka inaendelea kujengwa ili kukidhi mahitaji;
   (d) kiliwezesha uchimbaji wa visima kumi na viwili vya maji kwa lengo la kupata wastani wa lita 100,000 kwa saa. Mahitaji halisi ni lita 400,000 kwa saa;
   (e) kiligharimia ununuzi wa zana za kisasa za kufundishia na kujifunzia; na
   (f) kilifanya tathmini ya kitaalamu ili kuona maeneo yanayohitaji kuimarishwa katika utoaji wa elimu.

## Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

87. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kina majukumu ya kuendesha mafunzo katika fani za Sayansi za Jamii kwa kiwango cha Cheti, Stashahada na Shahada; kutoa mafunzo ya uongozi; kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa sekta ya umma na binafsi.

88. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2010/11 *Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere* kilitekeleza mambo yafuatayo:

(a) kilidahili wanachuo 1,212 (420 - Cheti, 320 - Stashahada na 472 - Shahada ya Kwanza), ambapo wanawake ni 742 ambayo ni sawa na asilimia 61.2 ya wanchuo wote;

(b) kiligharimia mafunzo ya wafanyakazi 14 ambapo 11 ni wanataaluma (Shahada ya Uzamivu 6, Shahada ya Uzamili 5), na 4 ni wafanyakazi waendeshaji (- Shahada ya Uzamili 1, Shahada ya Kwanza ya Ukutubi 2, na Stashahada ya Kawaida ya Ufundi 1);

(c) kilikamilisha tathmini ya mitaala ya programu za Cheti, Stashahada na Shahada ya Kwanza ili kuinua ubora wake. Mitaala hiyo imekwishawasilishwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na kuidhinishwa rasmi;

(d) kilikamilisha uandaaji wa mitaala ya ualimu kwa ajili ya programu za Stashahada na Shahada ya Kwanza. Mitaala hiyo imekwishawasilishwa NACTE kwa kuidhinishwa;

(e) kiliendelea na ujenzi wa Jengo lenye madarasa na ofisi kwenye Tawi la Chuo eneo la Bububu, Zanzibar, ambapo Jengo hilo litaanza kutumika katika mwaka wa fedha 2011/2012. Ujenzi huo unafanyika kwa awamu tatu; na

(f) kiliendelea kufuatilia katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la mmomonyoko wa ardhi ufukweni mwa Bahari ya Hindi, Kivukoni;

## Chuo cha Ufundi Arusha

89. **Mheshimiwa Spika,** *Chuo cha Ufundi Arusha* kina majukumu ya kutoa elimu na mafunzo ya ufundi katika fani za magari, ujenzi, mitambo, umeme, barabara, sayansi na teknolojia ya maabara, eletroniki na mawasiliano ya anga; kwa kiwango cha cheti na stashahada. Aidha, chuo hufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo yake ya taaluma na kitaalamu.

90. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2010/11, *Chuo cha Ufundi Arusha kilitekeleza mambo yafuatayo:*

(a) kilidahili jumla ya wanafunzi 357 wa mwaka wa kwanza ambapo kati yao 332 walidahiliwa katika ngazi ya stashahada na 25 katika ngazi ya Shahada;

(b) kiliendesha mafunzo ya Kozi ya Awali (Pre-Entry Course) kwa wanafunzi wa kike 64 kwa kushirikiana na Mfuko wa Elimu Tanzania (TEA);

(c) kiliandaa mitaala 4 mipya ya programu za Ufundi sanifu (NTAs 4 - 6) katika: Madini Vito na Usonara *(Lapidary and Jewellery Technology);* Ujenzi na Umwagiliaji (Civil and Irrigation Engineering); Magari na Mitambo Mikubwa *(Heavy Duty Equipment Technology);* na Umeme wa Magari na Elekroniki (Auto Electric and Electronics);

(d) kilikarabati bweni la wanafunzi wa kiume *(Hostel I);* ofisi 5 za watumishi/wanataaluma *(Shamba Building)* na nyumba 5 za watumishi wa Chuo;

(e) kiligharimia mafunzo ya muda mrefu kwa wanataaluma 14 (Shahada 4, Stashahada ya Uzamili 8 na Shahada ya Uzamivu 2);

(f) kilianza upanuzi wa jengo la Utawala;

(g) kilinunua gari moja aina ya pick-up ili kuinua ubora wa huduma za taaluma;

(h) kiliendeleza Ushirikiano na Chuo Kikuu cha Camosun cha nchini Canada kupitia mradi wa *Education for Employment* (EFE). Wanataaluma wanne (4) walipata mafunzo ya muda mfupi nchini Canada; na

(i) kiliendeleza ushirikiano na Vyuo vya Ufundi barani Afrika, chini ya uratibu wa *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa* (CAPA).

# V. CHANGAMOTO

91. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyooneshwa, katika ngazi mbalimbali, Wizara yangu ilikabiliana na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa malengo ya mwaka 2010/11. Zifuatazo ni baadhi ya changamoto hizo ni:

(a) kushuka kwa kiwango halisi cha uandikishaji wa rika lengwa *[Net Enrolment Ratio (NER)]* katika elimu ya msingi kutoka 95.9 mwaka 2009 hadi 95.4 mwaka 2010;

(b) uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo ya ufundi;

(c) upungufu wa walimu, wakufunzi na wahadhiri;

(d) uhaba wa madarasa, kumbi za mihadhara, maktaba, maabara na karakana;

(e) uhaba wa nyumba za walimu, wakufunzi na wahadhiri;

(f) kushuka kwa ufaulu wa kidato cha pili kutoka asilimia 65.3 mwaka 2009 hadi 61.8 mwaka 2010;

(g) kushuka kwa ufaulu wa kidato cha nne kutoka asilimia 72.5 mwaka 2009 hadi 50.2 mwaka 2010;

(h) ufinyu wa nafasi za kujiunga na elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ambapo idadi ya wahitimu wa elimu ya msingi na sekondari kwa mwaka ni 639,700 wakati nafasi za mafunzo ya ufundi na ufundi stadi ni 84,000 tu;

(i) upungufu wa rasilimali watu, miundombinu na fedha kulingana na ongezeko la uandikishaji na gharama katika ngazi zote za elimu;

(j) kushuka kwa idadi ya wananchi wanaoshiriki katika 'Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii' (MUKEJA) kutoka washiriki 957,289 mwaka 2009 hadi 924,893 mwaka 2010.

(k) kukosekana kwa mfumo unaowezesha kutambua na kutumia matokeo ya utafiti unaofanyika katika maeneo mbalimbali na kuwafikishia wadau matokeo yake;

(l) kuimarisha utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa kuoanisha taarifa zawakopeshaji na zile za Tume ya Vyuo Vikuu, Baraza la Mitihani na mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

## VI. MALENGO NA BAJETI YA MWAKA 2011/12

92. **Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mipango na Bajeti ya mwaka 2010/11, Wizara imejizatiti kutekeleza yafuatayo katika mwaka wa fedha 2011/12.

### Ofisi ya Kamishna wa Elimu

93. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2011/12, *Ofisi ya Kamishna* itatekeleza yafuatayo:

(a) kufanya uteuzi wa wanafunzi wenye ulemavu waliofaulu mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi kwa ajili ya kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2012;

(b) kuboresha utoaji wa Elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa kununua na kusambaza vifaa maalumu vya kufundishia na kujifunzia pamoja na visaidizi katika shule za Msingi na vitengo 317, shule 30 za Sekondari na vyuo vya ualimu 7;

(c) kuendelea kusimamia ubora wa vitabu vya kufundishia na kujifunzia katika Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu kwa kutoa ithibati ya vitabu;

(d) kutafsiri taarifa ya utafiti wa mradi wa SACMEQ III katika Kiswahili;

(e) kuandaa na kutangaza vipindi 576 vya redio kwa masomo ya Shule za Msingi;

(f) kuandaa na kutangaza vipindi 52 redioni kuhusu mbinu za ufundishaji;
(g) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa 'Elimu ya Mazingira' na 'Elimu kwa Maendeleo Endelevu';
(h) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa 'Kampeni ya Elimu kwa Wasichana';
(i) kuhamasisha menejimenti ya Wizara na wafanyakazi wengine kuhusu upimaji wa hiari wa VVU katika sehemu za kazi; na
(j) kufanya ufuatiliaji wa utoaji wa Huduma za Unasihi katika Kanda za Ziwa, Magharibi, Kusini, Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini - Magharibi na Nyanda za Juu.

## Idara ya Elimu ya Msingi

94. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2011/12 *Idara ya Elimu ya Msingi* itatekeleza yafuatayo:

(a) kutoa mwongozo na kuwajengea uwezo wasimamizi wa Elimu ya Awali na Msingi ngazi ya Mkoa na Halmashauri juu ya mwongozo wa viwango na uendeshaji wa Elimu ya Awali na Msingi;
(b) kuandaa 'Mwongozo wa Mafunzo Kazini kwa Walimu wa Elimu ya Awali';
(c) kuandaa 'Mwongozo wa Ufundishaji wa Walimu na Waendeshaji wa Elimu ya Awali kuhusu Upimaji na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Elimu ya Awali';
(d) kufuatilia uandikishaji wa watoto wote wa rika lengwa katika Elimu ya Awali na Msingi, mahudhurio na mikakati ya wanafunzi kubaki shuleni hadi kuhitimu;
(e) kufanya ufuatiliaji wa uendeshaji wa elimu ya awali na msingi, hususan katika upatikanaji na matumizi ya

vifaa sahihi vya kufundishia na kujifunzia, na ujenzi wa miundombinu ya shule ikiwemo vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na vyoo;

(f) kusimamia na kuratibu Awamu ya Pili ya MMEM na kukamilisha andiko la MMEM Awamu ya Tatu mwaka 2012-2016;

(g) kuratibu na kusimamia utoaji wa mafunzo kazini kwa walimu wa sayansi, hisabati na lugha ya kiingereza ili kuinua na kuimarisha kiwango cha taaluma katika elimu ya awali na msingi;

(h) kuandaa na kupima mafanikio ya ufundishaji na ujifunzaji na kuratibu uendeshaji wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la IV, Ufundi Stadi na Mtihani wa Taifa wa Kuhitimu Elimu ya Msingi;

(i) kufanya mapitio ya mtaala wa Elimu ya Msingi kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania, kwa lengo la kuinua ubora wa ufundishaji na kujifunza;

(j) kuratibu 'Mpango wa Lishe Shuleni' unaofadhiliwa na World Food Programme (WFP) na kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa 'Mpango wa Kitaifa wa Lishe Shuleni'; na

(k) kuhuisha miongozo ya uandikishaji kwa lengo la kufafanua na kusimamia majukumu ya kila mdau.

## Idara ya Elimu ya Sekondari

95. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2011/12, *Idara ya Elimu ya Sekondari* itatekeleza yafuatayo:

a) kutoa mafunzo kazini kwa walimu 2,500 wa masomo ya sayansi, hisabati, TEHAMA na *english;*

b) kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa njia ya

TEHAMA ikizingatia mazingira ya shule zetu za sekondari kwa kuanzia na shule 30 za majaribio;

c) kuendesha kambi za masomo ya sayansi kwa ajili ya wasichana ili kuwajengea uwezo wa kufaulu katika masomo hayo;

d) kuendesha programu za TUSEME kwa lengo la kuwawezesha wasichana kujiamini;

e) kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mashindano ya uandishi wa insha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Nchi za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika; na

f) kufuatilia taarifa za utekelezaji wa mitaala na tathmini ya ubora wa elimu ya sekondari katika ngazi ya Halmashauri.

## Idara ya Elimu ya Ualimu

96. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2011/12, *Idara ya Elimu ya Ualimu* itatekeleza yafuatayo:

(a) kudahili wanachuo 14,041 (Cheti 8,360, Stashahada 5,681) katika mafunzo ya Ualimu tarajali na kazini na kufanya idadi ya wanachuo wote kuwa 24,600;

(b) kuendesha mafunzo kazini kwa ajili ya walimu 2,052 wanaofundisha masomo ya sayansi, hisabati na lugha katika Shule za Msingi na Sekondari ili kuinua ubora wa ufundishaji wa masomo hayo;

(c) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu ya MWAKEM;

(d) kuendesha mafunzo kwa wakufunzi na walimu wanafunzi kuhusu matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza;

(e) kuendelea kusimamia na kuimarisha michezo katika vyuo 11 vya ualimu vya Serikali;

(f) kuimarisha miundombinu ya vyuo 10 vya Ualimu vya Serikali ili kuleta ufanisi katika utoaji wa elimu;

(g) kuinua ubora wa maabara za vyuo 3 vya Ualimu vya Serikali vyenye mchepuo wa Sayansi kwa kuvipatia vifaa na kemikali zinazotakiwa kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo katika vyuo hivyo; na

(h) kuimarisha uwezo wa wakufunzi na watendaji 30 wa idara na Vyuo vya Ualimu vya Serikali katika usimamizi wa 'Mkakati wa Menejimenti na Maendeleo ya Walimu' (MMEMWA).

## Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi

97. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi* itafanya yafuatayo:

(a) kuzindua mpango wa 'Ndiyo Ninaweza' kwa lengo la kufuta ujinga wa kutojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK);

(b) kuwezesha uandaaji na utoaji wa machapisho 21 ya magazeti vijijini, katika kanda saba za kisomo;

(c) kufanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu ufundishaji kwa kutumia mbinu shirikishi katika Halmashauri kumi za majaribio; mfumo wa habari na takwimu katika Halmashauri za Miji 12 na programu za EWW na ENMRA katika Halmashauri 132;

(d) kufuatilia na kutathmini majaribio katika Halmashauri 9 zilizo chini ya mpango wa 'Ndiyo Ninaweza' wa kufuta ujinga wa kutojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu;

(e) kuandaa mafunzo kwa wawezeshaji 50 wa mpango wa 'Ndiyo Ninaweza' kwa wanakisomo wenye mahitaji maalumu;

(f) kufanya utafiti ili kujua kiwango cha kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu katika Halmashauri zote nchini;
(g) kuratibu uandaaji wa utekelezaji wa mfumo unaoainisha sifa na viwango vya wahitimu wa mipango ya EWW na ENMRA; na
(h) kufanya tathmini ya utekelezaji wa 'Elimu kwa Wote' kuanzia mwaka 2000 hadi 2010.

## Idara ya Elimu ya Juu

98. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Idara ya Elimu ya Juu* itatekeleza yafuatayo:

(a) kugharimia mafunzo ya wanafunzi 1,900 (Madaktari wa Binadamu, Meno na Tiba ya Mifugo) kwenye vyuo vikuu vya ndani;
(b) kudhamini wanafunzi 50 raia wa Uganda wanaosoma kwenye vyuo vikuu hapa nchini na watanzania 76 wanaosoma Msumbiji chini ya utaratibu wa kubadilishana wanafunzi baina ya Tanzania na Uganda na Tanzania na Msumbiji;
(c) kuendelea kutekeleza mkataba wa ushirikiano kati ya Tanzania na China kwa kudhamini wanafunzi 5 raia wa China katika vyuo vikuu nchini;
(d) kuendelea kuelimisha umma kuhusu dhana ya uchangiaji wa gharama za Elimu ya Juu na fursa za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi, kupitia vyombo vya habari, maonesho ya taasisi za Elimu ya Juu na kutembelea wadau;
(e) kugharimia mahitaji maalum ya wanafunzi 112 wenye ulemavu katika vyuo vikuu nchini;
(f) kudhamini mafunzo ya shahada za uzamili kwa wanataaluma 80 katika vyuo vikuu vya umma;

(g) kudhamini mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu kwa wahadhiri 40 kupitia mpango wa DAAD;

(h) kuratibu uteuzi wa wanafunzi 190 kwa ajili ya nafasi zinazotolewa na nchi rafiki ambazo ni Algeria, China, Cuba, Urusi, Uingereza, Korea ya Kusini, Uturuki, Misri na India;

(i) kuandaa maandiko mradi ya utekelezaji wa MMEJU katika maeneo yafuatayo:
- ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vikuu vya umma;
- utafiti katika maeneo yaliyoainishwa katika Mpango wa Kitaifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano;
- uendelezaji wa wafanyakazi wanataaluma na waendeshaji;
- TEHAMA; na

(j) kuendelea kutekeleza mradi wa 'Sayansi na Teknolojia katika Elimu ya Juu' *(Science and Technology in Higher Education)* hasa katika ujenzi na mafunzo ya wanataaluma.

## Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi

99. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2011/12, *Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi* itatekeleza yafuatayo:

(a) kukamilisha 'Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi' (MMEU) na kuanza utekelezaji wake;

(b) kuratibu zoezi la kuvijengea uwezo vyuo 15 vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika utoaji wa Elimu inayozingatia umahiri, uchambuzi wa mahitaji ya soko la ajira na masuala ya utafiti kwa kushirikiana na 'Umoja

wa Vyuo Jamii vya Canada' *(Association of Canadian Community Colleges);*

(c) kuratibu zoezi la kufanya uchambuzi wa mahitaji ya stadi katika wilaya 15 ambazo hazina vyuo vya Ufundi Stadi;

(d) kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(e) kukamilisha uhuishaji wa mipango, mikakati na miongozo ya utekelezaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(f) kuratibu uanzishwaji wa vyuo vya ufundi stadi vya wilaya; na

(g) kuratibu ukamilishaji wa ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya mikoa ya Lindi, Manyara, Pwani na Dar es Salaam na cha wilaya ya Makete.

## Idara ya Ukaguzi wa Shule

100. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Idara ya Ukaguzi wa Shul*e itatekeleza yafuatayo:

(a) kusimamia ubora wa elimu itolewayo kwa kukagua jumla ya Asasi za Elimu 20,045;

(b) kusimamia, kuendesha na kufanya tathmini ya kiwango cha ufaulu wa mtihani wa kidato cha 2 mwaka 2011 kwa kushirikiana na Idara ya Elimu ya Sekondari;

(c) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za ukaguzi wa shule katika ngazi za kanda na Wilaya; na

(d) kutoa mafunzo kwa wakaguzi 70 wa shule ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa elimu.

## Idara ya Sera na Mipango

101. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Idara ya Sera na Mipango* itatekeleza yafuatayo:
   (a) kukamilisha na kuandaa Mikakati na Miongozo ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo;
   (b) kuwasilisha, kwa wadau, Sera ya Elimu na Mafunzo iliyohuishwa na kutoa elimu juu ya utekelezaji wake;
   (c) kuendelea kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa takwimu na taarifa za elimu kwa kugatua mfumo wa ukusanyaji Takwimu *(Database)* kwenda kwenye Halmashauri 40 chini ya Awamu ya Pili ya MMES 2010 - 2015;
   (d) kuandaa Mkutano wa Pamoja wa Mapitio ya Sekta ya Elimu (Joint Education Sector Review) wa mwaka 2011 unaoshirikisha wadau wa elimu;
   (e) kuendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya elimu katika ngazi zote;
   (f) kufanya mapitio ya Mpango-Mkakati wa Wizara (Ministerial Strategic Plan) na kuandaa Mpango wa Wizara wa miaka mitano unaolingana na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano; na
   (g) kuandaa Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Fedha ya Umma *(Medium Term Expenditure Framework)* wa miaka mitano kutokana na Mpango wa Wizara wa Maendeleo wa miaka mitano.

## Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu

102. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2011/12, *Idara ya Utawala na Rasilimaliwatu* itatekeleza yafuatayo:
   (a) kuimarisha usimamizi wa utoaji huduma bora za elimu kwa kuajiri watumishi wapya 833, kutoa vibali vya wataalamu

wa kigeni 800, kuratibu upandishaji vyeo wa watumishi 917 na uthibitishaji kazini wa watumishi 351;

(b) kuratibu utekelezaji wa Mkataba Mpya wa Huduma kwa Mteja;

(c) kuratibu tathmini ya utendaji kazi wa watumishi kwa njia ya wazi (OPRAS) kuanzia mwezi Julai, 2011; na

(d) kuanza kutumia mfumo wa kompyuta wa kuhifadhi taarifa zote za kiutumishi kwa wafanyakazi wote wa Wizara.

## Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano

103. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano* kitatekeleza yafuatayo:

(a) kuratibu utoaji wa habari katika vyombo vya habari kuhusu matukio mbalimbali ya sekta ya Elimu ili kuufahamisha Umma kuhusu maendeleo ya sekta ya Elimu na kuweka kumbukumbu za matukio ya Wizara;

(b) kukamilisha 'Mkakati wa Mawasiliano na Habari' unaohusu shughuli za Wizara;

(c) kuandaa na kutangaza vipindi 20 vya redio na televisheni vya kuelimisha jamii kuhusu maendeleo na changamoto za sekta ya elimu;

(d) kuandaa makala 20 juu ya matukio ya sekta ya Elimu, kwa ajili ya kuzichapisha katika magazeti;

(e) kuratibu upatikanaji wa majibu ya maswali yanayoulizwa na wadau wa elimu kupitia Tovuti ya Wananchi (www.wananchi.go.tz);

(f) kuandaa, kuchapa na kusambaza nakala 100,000 za Jarida la EdSDP kwenye kanda 8 za Elimu ili kuihamasisha jamii kushiriki katika kutekeleza mipango ya Elimu;

(g) kuandaa machapisho mbalimbali yakiwemo mabango, vipeperushi, vijarida, shajara na kalenda kwa ajili ya

kuwaeleza wadau juu ya sera na mipango mbalimbali ya maendeleo ya Elimu; na

(h) kuandaa na kuratibu maadhimisho ya miaka 50 ya uhuru.

## Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

104. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2011/12 *Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani* kitatekeleza yafuatayo:

(a) kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa mapendekezo ya Ukaguzi Makao Makuu ya Wizara, vituo 30 vikiwemo vyuo vya ualimu, ofisi za kanda za Ukaguzi wa Shule na Vituo vya Elimu vya Wizara.

## Kitengo cha Ununuzi na Ugavi

105. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2011/12 *Kitengo cha Ununuzi na Ugavi* kitatekeleza yafuatayo:

(a) kuandaa mpango wa Manunuzi wa Wizara kwa mwaka 2011/12 kwa kuzingatia Bajeti iliyopitishwa;

(b) kuhakikisha kuwa manunuzi ya Wizara yanafanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu zilizopo;

(c) kuhesabu mali kwa ajili ya kufunga mwaka wa fedha na kubaini na kushughulikia vifaa vinavyostahili kufutwa;

(d) kuandaa mafunzo juu ya sheria na taratibu za Manunuzi ya Umma kwa wajumbe wa Bodi ya Zabuni pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo;

(e) kuweka kumbukumbu sahihi za vifaa na mali za Wizara; na

(f) kutangaza zabuni na matokeo yake kwenye magazeti na Tovuti ya *Public Procurement Regulatory Authority* (PPRA).

## Kitengo cha Fedha na Uhasibu

106. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2011/12 *Kitengo cha Fedha na Uhasibu* kitatekeleza yafuatayo:
   (a) kuandaa ripoti mbalimbali za fedha na kuziwasilisha kwa mamlaka husika;
   (b) kuchambua ripoti za Mkaguzi wa Nje na Mkaguzi wa Ndani na kuratibu majibu ya hoja za ripoti ya ukaguzi kabla ya kuyawasilisha kwenye Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali;
   (c) kuhakikisha ya kuwa malipo yanafanywa kwa kuzingatia taratibu, kanuni na sheria za manunuzi na Fedha za Umma; na
   (d) kusimamia na kushauri kuhusu Makusanyo ya Maduhuli.

## WAKALA, TAASISI NA MABARAZA YA WIZARA

107. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2011/12, kila Wakala, Baraza na Taasisi zitatekeleza kazi zake kama ifuatavyo:

## Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

108. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2011/12, *Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima* (TEWW) itatekeleza yafuatayo:
   (a) kutoa mafunzo ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelezi kwa kutumia Competence Based Education & Training Curriculum (CBET), kwa walengwa 140 wa ngazi ya Cheti, 300 wa Stashahada na 352 wa Shahada;
   (b) kudurusu mtaala wa CBET ngazi ya cheti, stashahada na shahada na kuwajengea uwezo wakufunzi wa TEWW katika kutoa mafunzo yanayozingatia uwezo na umahiri;

(c) kutekeleza mpango mkakati wa UKIMWI wa TEWW *(HIV and AIDS Work Place Strategy);*

(d) kufanya utafiti juu ya programu zinazotolewa na taasisi ili kubaini umuhimu wake katika jamii;

(e) kutoa machapisho na majarida ya kitaaluma ya Journal of Adult Education No.19 na Studies in Adult Education No.67;

(f) kujenga vyumba vya semina na kumbi za mikutano katika kituo cha WAMO, ofisi na madarasa katika mikoa ya Kilimanjaro, Ruvuma na Arusha na kukarabati jengo la makao makuu ya taasisi na kujenga hosteli ya wanafunzi katika Mkoa wa Dar es Salaam;

(g) kuunganisha makao makuu ya taasisi na vituo vitano katika mtandao wa mawasiliano ya kompyuta kwa ajili ya kuinua ubora wa utoaji wa Elimu Masafa;

(h) kuendesha mafunzo ya uratibu, usimamizi na menejimenti ya vituo vya MEMKWA na MUKEJA katika wilaya 75 zilizobaki;

(i) kuratibu maandalizi ya mkutano wa Elimu Masafa katika nchi za SADC *(DEASA Conference)* utakaofanyika Tanzania;

(j) kuchapa masomo ya Hatua ya I na II ya 'Mpango wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana';

(k) kuandika na kuchapa kwa mtindo wa moduli masomo ya Ufundi na Biashara kwa ajili ya kidato cha 5 na 6;

(l) kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma kupitia 'Mpango wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana' kutoka 49,533 hadi 69,533;

(m) kuratibu utekelezaji wa Programu ya *Integrated Post-Primary Education* (IPPE) katika wilaya za Temeke, Magu, Siha, Hai, Bagamoyo, Makete na Mtwara; na

(n) kuratibu mafunzo ya Diploma ya Elimu ya Watu Wazima

na Maendeleo ya Jamii kwa njia ya Elimu masafa kwa Wakufunzi wa vyuo vya maendeleo ya jamii (FDC) kwa ushirikiano na Karibu Tanzania Association (KTA) na Karibu Sweden Association (KSA).

## Taasisi ya Elimu Tanzania

109. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Taasisi ya Elimu Tanzania* itatekeleza yafuatayo:
   (a) kufanya mapitio ya mitaala ili kuinua ubora wa elimu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu;
   (b) kutoa mafunzo ya kubuni na kutekeleza mtaala ngazi ya cheti na shahada; na
   (c) kujenga kituo cha mafunzo ya mtaala na utafiti wa maendeleo ya elimu.

## Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania

110. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania* itatekeleza yafuatayo:
   (a) kuimarisha na kuinua ubora wa huduma za Maktaba kwa watu wazima na watoto katika mikoa 19, kwa kuongeza machapisho 50,000;
   (b) kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba za shule, vyuo, taasisi na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya nchini;
   (c) kutoa mafunzo ya ukutubi na uhifadhi nyaraka kwa walengwa 200 wa cheti, 200 wa stashahada na 150 wa mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya wafanyakazi wa maktaba za umma, shule, vyuo na taasisi nyingine nchini; na

(d) kuendeleza ujenzi na kuimarisha Chuo cha Mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka *(School of Library, Archives and Documentation Studies - SLADS)* Bagamoyo, kwa kuanza ujenzi wa hosteli.

## Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)

111. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu* utatekeleza yafuatayo:

(a) kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa viongozi 600 wa idara mbalimbali za elimu, walengwa wakiwa ni Walimu Wakuu, Waratibu Elimu Kata, Maafisaelimu ngazi ya Wilaya, walimu wa Shule za Awali, Msingi na Sekondari, wafanyakazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na mameneja na wamiliki wa shule zisizo za serikali;

(b) kutoa mafunzo ya mwezi mmoja ya 'Cheti cha Uongozi na Uendeshaji wa Elimu' kwa Walimu Wakuu 1,000;

(c) kutoa mafunzo kwa Waratibu Elimu Kata 2,800 nchini kote juu ya mbinu bora za kusimamia Elimu ya Sekondari katika kata zao;

(d) kutoa mafunzo kwa wajumbe 5,000 wa Kamati za Shule juu ya usimamizi wa Elimu ya Msingi;

(e) kutoa mafunzo kwa wajumbe 1,500 wa Bodi za Shule juu ya usimamizi na uendeshaji wa Shule za Sekondari;

(f) kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Maafisa Elimu Taaluma na Maafisa Elimu Vifaa na Takwimu 86 juu ya usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini;

(g) kutoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na uendeshaji wa elimu kwa Wakuu wa Shule 240 wa shule za serikali na zisizo za serikali;

(h) kutoa mafunzo ya awali ya uongozi na uendeshaji wa

elimu kwa Wakuu wa Shule wapya 1,000 kutoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara;

(i) kutoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na uendeshaji wa elimu kwa wakaguzi 240 kutoka Wilaya zote za Tanzania Bara; na

(j) kutoa mafunzo ya uongozi na uendeshaji wa elimu kwa Maafisa Elimu 106 wa Wilaya na Mikoa ya Tanzania Bara.

## Tume ya Taifa ya UNESCO

112. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Tume ya Taifa ya UNESCO* itatekeleza yafuatayo:

(a) kuratibu ushiriki wa serikali katika kikao cha 35 cha Mkutano Mkuu wa UNESCO utakaofanyika Oktoba 2011 Paris Ufaransa Makao Makuu ya UNESCO, pamoja na utekelezaji wa maamuzi ya kikao hicho;

(b) kuratibu uanzishwaji wa 'Kikundi cha Wanawake katika Sayansi Tanzania' (STI4W Reference Group) ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika sayansi na ubunifu;

(c) kuendelea kusimamia utekelezaji wa 'Programu ya Ushirikishwaji' ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa 'Kituo cha Taifa cha Utafiti na Uhifadhi wa Nyaraka za Masuala ya Jinsia', Tengeru -Arusha;

(d) kuratibu ushiriki wa vijana katika utekelezaji wa programu za UNESCO, kupitia 'Dawati la Vijana la Tume ya Taifa ya UNESCO';

(e) kuhamasisha shule nyingi zaidi kujiunga na mtandao wa UNESCO katika kutekeleza Programu za UNESCO; na

(f) kuratibu mchakato wa taifa wa kuridhia Mkataba wa UNESCO kuhusu 'Kupinga Utumiaji wa Dawa za Kuongeza Nguvu Michezoni' *(Convention on Antidoping in Sports)*.

## Baraza la Mitihani la Tanzania

113. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Baraza la Mitihani la Tanzania* litatekeleza yafuatayo:

(a) kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi 2011 kwa watahiniwa 992,795 waliosajiliwa;

(b) kuendesha Mitihani ya Kidato cha Nne, Maarifa (Qualifying Test- QT), Kidato cha Sita na Ualimu, ambapo watahiniwa wanatarajiwa kusajiliwa kwa ajili ya mitihani hiyo;

(c) kutoa mafunzo kwa walimu wanaoshiriki katika kazi za Baraza la Mitihani ili kuongeza ufanisi katika utungaji wa maswali ya mitihani; na

(d) kutoa mafunzo kwa maafisaelimu wa Mikoa na Wilaya juu ya matumizi ya karatasi za OMR (Optical Mark Reader) katika kujibu maswali ya mtihani, ili kuongeza ufanisi katika shughuli za usahihishaji mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi.

## Kituo cha Maendeleo Dakawa

114. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12 *Kituo cha Maendeleo Dakawa* kitatekeleza kazi zifuatazo:

(a) kuendelea kutunza na kuhifadhi kumbukumbu za historia ya ukombozi Kusini mwa Afrika;

(b) kuendelea na mchakato wa kukifanya Kituo kuwa kitovu cha utoaji wa elimu ya Sayansi na Ufundi *(Centre of Excellence);* na

(c) kuandaa mpango wa kisheria wa uendeshaji wa Kituo.

## Mamlaka ya Elimu Tanzania

115. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2011/12, *Mamlaka ya Elimu Tanzania* itatekeleza yafuatayo:

(a) kuendesha harambee kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 30 ya wasichana wa shule za Sekondari;

(b) kuendelea kuimarisha miundombinu ya shule za sekondari 197 na vyuo vya elimu ya juu 3 kwa kufadhili miradi ya maboresho;

(c) kufanya tathmini na ukaguzi wa miradi 70 inayofadhiliwa na Mfuko wa Elimu;

(d) kuwapatia mafunzo watumishi 30 wa Mamlaka ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi; na

(e) kukarabati majengo yatakayokuwa ofisi za Mamlaka.

## Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania

116. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2011/12, *Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania* itatekeleza yafuatayo:

(a) kutathmini ubora wa programu 100 za masomo ya Vyuo Vikuu na vyuo vikuu vishiriki nchini kwa lengo la kuziidhinisha;

(b) kuendesha warsha na semina 5 za kuwajengea uwezo viongozi wa vyuo vikuu ili kuinua ubora wa uongozi wa vyuo vikuu nchini;

(c) kukamilisha rasimu ya kanuni za utekelezaji wa Mfumo wa Tuzo Zinazotambuliwa Kitaifa *(National Qualifications Framework);*

(d) kuendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uwezo wa vyuo vikuu vilivyopo na vipya katika kutoa elimu bora kwa kuzingatia vigezo na kutumia takwimu na taarifa mbalimbali toka vyuo vikuu kwa ajili ya kusaidia kutoa

maamuzi sahihi kwa ajili ya maendeleo ya elimu ya juu nchini;

(e) kuendelea kuratibu na kutathmini mradi wa majaribio ya udhibiti wa ubora wa programu za vyuo vikuu 5 unaotekelezwa na IUCEA;

(f) kuelimisha umma kuhusu majukumu ya Tume, kupitia machapisho mbalimbali na vyombo vya habari na kutoa miongozo kwa vyuo vikuu nchini kuhusu udhibiti wa ubora wa elimu ya juu;

(g) kuendelea kuratibu na kusimamia udahili wa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu nchini na nje ya nchi;

(h) kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi za kudumu za Tume;

(i) kuendelea kuratibu na kuandaa maonesho ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ili kuuelimisha umma kuhusu malengo, maendeleo na mchango wa taasisi za elimu ya juu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini; na

(j) kujenga uwezo wa wafanyakazi wa Tume katika kukabiliana na changamoto za maendeleo ya elimu ya juu kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

## Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi

117. **Mheshimiwa Spika,** mwaka 2011/12, *Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi* litatekeleza yafuatayo:

(a) kukagua vyuo 20 na kutoa ithibati na usajili kwa vyuo vinavyostahili;

(b) kubaini na kusajili walimu 400 katika Vyuo vya Ufundi;

(c) kuratibu mitaala 30 na uendeshaji wa mitihani katika vyuo 30;

(d) kusimamia vyuo 20 katika kutengeneza mfumo wa kudhibiti na kuhakiki ubora wa mafunzo;

(e) kuratibu udahili wa wanafunzi wa shahada na stashahada

katika vyuo 17;

(f) kusimamia utekelezaji wa masharti ya ithibati katika vyuo; na

(g) kuendesha mafunzo ya walimu katika vyuo 20 juu ya kufundisha kwa kutumia mitaala mipya.

## Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

118. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu* itatekeleza yafuatayo:

(a) kutoa mikopo kwa Wanafunzi 91,568 wa elimu ya juu wa mwaka wa kwanza na wale wanaoendelea na masomo, na kwa wanafunzi wanaosoma shahada za uzamili na uzamivu;

(b) kuimarisha utoaji na urejeshaji mikopo kwa kuoanisha taarifa za wakopeshwaji na zile za Tume ya Vyuo Vikuu, Baraza la Mitihani na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;

(c) kutoa Elimu kwa Umma, kwa kutumia vipeperushi, magazeti, redio, televisheni, warsha na maonesho, kuhusu kuchangia gharama za Elimu ya Juu; na

(d) kusogeza huduma za utoaji wa mikopo karibu na wananchi kwa kuanzisha Ofisi ya Kanda huko Zanzibar.

## Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

119. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2011/12, *Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi* itatekeleza yafuatayo:

(a) kukamilisha andiko la 'Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Ufundi Stadi wa Miaka Mitano' *(VETA Development Corporate Plan IV)* 2012-2017;

(b) kuendelea kuimarisha utekelezaji wa awamu ya kwanza ya 'Programu ya Vituo vya Ufundi Stadi vya Wilaya' *(District*

*Vocational Training Centres Programme)* kwa kukarabati vituo na kujenga vituo vya ufundi stadi katika wilaya za Karagwe, Korogwe, na Mwanga na kujenga chuo Ludewa. Kituo cha Ufundi cha Wilaya ya Makete ambacho ujenzi wake unatarajiwa kukamilika hivi karibuni kitaanza kutoa mafunzo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/12;

(c) kujenga uwezo wa wakufunzi 70 na watumishi wa kawaida 50 katika vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi;

(d) kufanya utafiti wa soko la ajira nchi nzima ili kubaini mahitaji ya mafunzo ya ufundi stadi kisekta, hususan stadi zinazohitajika na wawekezaji (Potential and Emerging skills);

(e) kutekeleza mpango wa mafunzo ya ufundi viwandani uitwao *Skills Enhancement Programme* (SEP) kwa kampuni zisizopungua 10 nchi nzima, ili kuimarisha stadi kwa wafanyakazi na tija kwa viwanda husika;

(f) kutekeleza Mpango wa VETA wa kuimarisha vyuo vya Ufundi Stadi *(Modernization of Vocational Training Centres)* kwa kukarabati vyuo vya mafunzo ya Ufundi Stadi vya Mwanza, Moshi, Mtwara, Kihonda na Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi cha Morogoro pamoja na kuweka mitambo ya kisasa ya kufundishia ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia;

(g) kuanzisha mafunzo ya hoteli na utalii katika chuo cha VETA cha Hoteli na Utalii huko Njiro, Arusha ambapo wanafunzi 50 wa ngazi ya Stashahada wataanza Mafunzo mwezi Januari, 2012; na

(h) kuanzisha mafunzo ya ufundi stadi katika fani za useremala, uashi, magari, umeme, upishi na TEHAMA katika vyuo vipya vya Manyara, Lindi, Pwani na kituo cha TEHAMA cha Kipawa jijini Dar es Salaam.

## Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

120. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2011/12, *Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* kitatekeleza yafuatayo:

(a) kudahili wanafunzi 7,260 ambapo, 5,030 ni wa shahada ya kwanza na 2,230 ni wa shahada ya uzamili na uzamivu;

(b) kuendeleza ushirikiano na wafadhili mbalimbali katika kugharimia utafiti na mafunzo, hasa katika nyanja za sayansi asilia na tumizi *(Natural and Applied Sciences)*, teknolojia, elimu, mabadiliko ya tabianchi, miundombinu, mazingira, ujasiriamali, nishati, utalii, sekta isiyo rasmi, TEHAMA, lugha, utawala bora na demokrasia, na baadaye kutoa machapisho 30 ya vitabu na 305 ya majarida;

(c) kuendeleza ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya chuo ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(d) kuendeleza mikakati ya ujenzi wa makao makuu mapya ya Taasisi ya Sayansi za Bahari eneo la Buyu, Zanzibar.

(e) kuanzisha shahada za kwanza za B.Sc. in Textile Engineering, na B.Sc. in Textile Design;

(f) kukamilisha na kuanzisha shahada nne za uzamivu *(PhD by Coursework and Dissertation)* katika Taasisi ya za Taaluma za Maendeleo, Idara ya Sayansi za Bahari, Idara ya Zuolojia na Fani ya Sayansi za Jamii;

(g) kuendelea kufanya ukaguzi wa ubora wa shughuli za taaluma *(quality assurance)*;

(h) kuendelea kuajiri na kugharimia mafunzo ya wahadhiri na wafanyakazi waendeshaji kwenye fani mbalimbali;

(i) kuendelea na utekelezaji wa mipango ya kusherehekea miaka 50 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kutathmini na kuandaa Dira ya Miaka 50 ijayo ya Chuo kuendesha midahalo, makongamano, na kutoa machapisho na huduma kwa umma; na

(j) kuanza ujenzi wa Kituo cha Wanafunzi *(Student Centre)* ikiwa ni azma mojawapo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kusherehekea miaka 50 ya Chuo.

## Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam)

121. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam* kitatekeleza yafuatayo:

(a) kudahili wanafunzi wenye sifa za kujiunga na masomo ya Chuo Kikuu 1,200 (200 wa fani ya sayansi);

(b) kununua vifaa vya maabara na samani za maktaba na vitabu zaidi vya kufundishia;

(c) kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia wanafunzi wenye ulemavu;

(d) kujenga jengo la kitivo cha sayansi za jamii;

(e) kupanua jengo la kitivo cha Elimu kwa ajili ya kuongeza ofisi kwa walimu;

(f) kujenga jengo la utawala kwa ajili ya ofisi za wafanyakazi waendeshaji;

(g) kuimarisha miundombinu ya TEHAMA;

(h) kushirikiana na vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hasa kwa shahada za uzamili na uzamivu;

(i) kujenga kituo cha afya ili kuwa na jengo maalum la kutolea huduma za afya;

(j) kujenga jengo la maabara na madarasa katika shule ya sekondari ya mazoezi;

(k) kuajiri jumla ya wafanyakazi 75; kati ya hao, 30 ni wahadhiri na 45 ni waendeshaji;

(l) kukarabati miundombinu ya umeme, barabara na viwanja vya michezo;

(m) kuzuia mmomonyoko wa udongo katika hosteli ya Mbagala; na

(n) kutengeneza Master Plan ya chuo na kununua/kutafuta ardhi nyingine kubwa kwa ajili ya upanuzi wa chuo.

## Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam)

122. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2011/12, *Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa* kitatekeleza yafuatayo:

(a) kuongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza kutoka 880 hadi 950.

(b) kuanza ujenzi wa jengo la Utawala;

(c) kuendelea kuimarisha kupanua miundombinu ya kufundishia na kujifunzia Chuoni; na

(d) kuendelea kugharimia masomo ya wahadhiri katika viwango vya uzamili na uzamivu.

## Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo

123. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2011/12, *Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo* kitatekeleza yafuatayo:

(a) kudahili wanachuo 8,572 wa shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu;

(b) kujenga na kukarabati miundombinu ya chuo ili kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(c) kuanzisha shahada mpya 7 za kwanza na 3 za Uzamili;

(d) kuanza mradi wa uvunaji maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji;

(e) kuanzisha Taasisi ya Kitaifa ya Bioteknolojia ya Kilimo *(National Agrilcultural Biotechnology Institute)* ili kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa 'Kilimo Kwanza'; na

(f) kufanya utafiti unaolenga katika kumwondolea mkulima umaskini, kukuza uchumi na kuboresha mazingira.

## Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Elimu ya Biashara Moshi (Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo)

124. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Elimu za Biashara Moshi* kitatekeleza kazi zifuatazo:

(a) kuanzisha programu za cheti na stashahada katika Kampasi ya Kizumbi, Shinyanga ili kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 3,652 mwaka 2010/11 hadi 4,068 mwaka 2011/12;

(b) kuwaendeleza wahadhiri 20 katika kiwango cha Shahada ya Uzamivu;

(c) kuinua ubora wa utafiti na kuandaa makala mbalimbali ili kusambaza elimu inayokidhi mahitaji ya sasa ya jamii, ikiwa ni pamoja na vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS), maendeleo ya ushirika, utunzaji mazingira, na upunguzaji wa umaskini;

(d) kuimarisha matawi manne ya chuo ya kanda katika mikoa ya Mtwara, Iringa, Mwanza na Tanga.

(e) kuinua ubora wa kiwango cha huduma za utafiti na ushauri, kwa kushirikiana na vyuo vingine vya ndani na nje ya nchi, hususan Chuo cha Ushirika cha Uingereza, University of Stirling cha Uingereza, Chuo Kikuu cha Malawi, Chuo Kikuu cha Zambia, Humber Institute of Technology and Advanced Learning (HITAL);

(f) kuimarisha mipango ya uenezi wa elimu nje ya Chuo ili kuchochea ari ya maendeleo katika jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, hususan Wizara ya Kilimo, Chakula na

Ushirika, Co-operative Audit and Supervision Corporation (COASCO), Muungano wa Vyama vya Ushirika (TFC) na wengineo;

(g) kushughulikia mahitaji ya jamii katika masuala mtambuko kama jinsia, UKIMWI, wenye ulemavu, rushwa, mazingira na wastaafu; na

(h) kukamilisha utekelezaji wa masharti yaliyotolewa na Tume ya Vyuo Vikuu ili kukiwezesha Chuo kupanda daraja na kuwa Chuo Kikuu kamili *(Fully Fledged University)*.

## Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

125. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2011/12, *Chuo Kikuu Huria cha Tanzania* kimejizatiti kutekeleza shughuli zifuatazo:

(a) kujenga maabara za Teknolojia ya Mawasiliano Huria katika mikoa ya Dodoma, Tabora, Pemba, Lindi, Mtwara, Mara na Zanzibar;

(b) kujenga majengo ya kituo cha Mtwara na viwanja vya michezo eneo la Makao Makuu ya Chuo Bungo Kibaha;

(c) kukarabati majengo ya Mikoa ya Kagera (Awamu II), Musoma (Awamu ya I) Kilimanjaro (Awamu ya II) na Rukwa (Awamu ya II); na

(d) kuongeza udahili wa wanafunzi ili ifikie 3,961 kwa shahada ya kwanza na 2,538 kwa shahada za uzamili na uzamivu;

## Chuo Kikuu Ardhi

126. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2011/12, *Chuo Kikuu Ardhi* kitatekeleza yafuatayo:

(a) kukamilisha awamu ya 5 ya ujenzi wa jengo la kumbi za mihadhara na ofisi za wahadhiri *(Lands Building);*

(b) kuanza ujenzi wa jengo la mihadhara na ofisi za wahadhiri;
(c) kuanza ujenzi wa hosteli ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,048;
(d) kuanza ujenzi wa nyumba ya Makamu Mkuu wa Chuo;
(e) kukamilisha ununuzi wa ardhi kwa ajili ya upanuzi wa chuo katika kijiji cha Lupunga, eneo la Mlandizi – Halmashauri ya Mji wa Kibaha;
(f) kuimarisha na kupanua miundombinu ya habari, mawasiliano na teknolojia;
(g) kuajiri wafanyakazi wapya 37 (wanataaluma 22 na waendeshaji 15); na
(h) kukarabati barabara za ndani, madarasa, ofisi za walimu, nyumba za wafanyakazi na viwanja vya michezo.

## Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili

127. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2011/12, *Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili* kitatekeleza yafuatayo:
(a) kudahili wanafunzi wapya 400 wa shahada ya kwanza na 250 wa shahada za uzamili na uzamivu;
(b) kujenga miundombinu ya barabara, maji na umeme katika eneo la Mloganzila ili kuwezesha kuanza kwa ujenzi wa hospitali ya kufundishia;
(c) kukamilisha ukarabati wa majengo yakiwemo ya utawala, nyumba za wafanyakazi, maabara za kufundishia na mabweni;
(d) kujenga nyumba mbili za walezi wa wanafunzi *(wardens)* na Bazaar ya wanafunzi katika mabweni ya wanafunzi yaliyopo Barabara ya Chole Dar es Salaam;
(e) kujenga karakana ya kutengenezea vifaa vya maabara;
(f) kuweka majiko ya gesi na samani katika mgahawa wa wafanyakazi katika jengo jipya;

(g) kufuatilia na kutathmini matumizi na ufanisi wa dawa za malaria katika jamii;

(h) kuendelea kufanya utafiti wa chanjo ya ukimwi kwa watu mia moja na ishirini (120) kama jaribio la pili. Utafiti huu utaratibiwa katika mikoa ya Dar es Salaam na Mbeya;

## Chuo Kikuu Mzumbe

128. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, C*huo Kikuu Mzumb*e kitatekeleza kazi zifuatazo:

(a) kudahili wanafunzi 3,455; kati yao, wanafunzi 1,460 wa Shahada ya Kwanza na 1,795 Shahada za Uzamili;

(b) kukamilisha ujenzi wa maktaba ya kampasi ya Mbeya yenye uwezo wa kuchukua wasomaji 600 kwa wakati mmoja;

(c) kuweka samani katika hosteli ya wanafunzi wa kike katika Kampasi Kuu Mzumbe;

(d) kujenga vyumba vitatu vya madarasa katika Kampasi ya Mbeya;

(e) kuimarisha mfumo wa maji katika Kampasi Kuu ya Mzumbe;

(f) kukamilisha utafiti na kutoa ushauri mbali mbali katika maeneo ya menejimenti, uongozi na Sayansi za Jamii kwa ujumla;

(g) kuajiri wahadhiri 14 na waendeshaji 8; na

(h) kugharimia mafunzo ya watumishi 18 katika ngazi ya Shahada za Uzamivu na 12 katika ngazi ya Shahada za Uzamili.

## Chuo Kikuu cha Dodoma

129. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Chuo Kikuu cha Dodoma* kitatekeleza yafuatayo:
    (a) kukamilisha ujenzi wa barabara za ndani;
    (b) kuanza ujenzi wa Chuo cha Sayansi za Asili (kwa ajili ya wanafunzi 5,000) na Chuo cha Sayansi za Ardhi (kwa ajili ya wanafunzi 3,000);
    (c) kuanza ujenzi wa awamu ya pili ya Chuo cha Elimu (Walimu wanafunzi 10,000), chuo cha Sayansi za Tiba (wanafunzi 4,500) na chuo cha Sayansi za kompyuta (wanafunzi 3,000);
    (d) kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya maji-safi na maji-taka.
    (e) kuhadili wanafunzi 5,000 kwenye shahada ya kwanza na 600 shahada za uzamili; na
    (f) kuendeleza utafiti katika maeneo mbalimbali ya mazingira, uchumi na tabianchi.

## Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

130. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere* kitatekeleza yafuatayo:
    (a) kudahili wanafunzi wapya 450 wa programu ya Cheti, *(wanafunzi 350 wa Stashahada na wanafunzi 490 wa Shahada ya Kwanza);*
    (b) kugharimia mafunzo ya wanataaluma 10 na wafanyakazi waendeshaji 10 ikiwa ni pamoja na wanaoendelea na masomo;
    (c) kuendelea kufuatilia katika Ofisi ya Makamu wa Rais *(Mazingira)* ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la mmomonyoko wa ardhi unaotishia kubomoa baadhi ya majengo ya chuo,

ufukweni mwa Bahari ya Hindi;
(d) kuanza ujenzi wa hosteli mbili za wanafunzi katika kampasi ya Kivukoni;
(e) kuendeleza ujenzi katika kampasi ya Bububu- Zanzibar ;
(f) kuajiri wanataaluma 15 na wafanyakazi waendeshaji 10; na
(g) kuanza mafunzo ya ualimu katika programu za Stashahada na Shahada ya Kwanza.

## Chuo cha Ufundi Arusha

131. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2011/12, *Chuo cha Ufundi Arusha* kitatekeleza yafuatayo:
(a) kudahili jumla ya wanafunzi 472 wa mwaka wa kwanza; kati ya hao, 447 ni ngazi ya Cheti na Stashahada na 25 ni ngazi ya Shahada;
(b) kuanzisha programu nne (4) za ufundi sanifu (NTAs 4-6) katika: Teknolojia ya Madini ya Vito na Usonara *(Lapidary and Jewellery Technology);* Uhandisi-Ujenzi na Umwagiliaji *(Civil and Irrigation Engineering);* Magari na Mitambo Mikubwa *(Heavy Duty Equipment Technology)* na Umeme wa Magari na Elekroniki *(Auto Electric and Electronics);*
(c) kununua vifaa na zana za kisasa za kufundishia na kujifunzia katika maabara na karakana ili kuinua ubora wa ufundishaji na ujifunzaji;
(d) kuhuisha mitaala 18 ya programu zilizopo za ufundi sanifu (NTAs 4-6);
(e) kuajiri wanataaluma 40 na wafanyakazi waendeshaji 30;
(f) kuendesha kozi ya awali *(Pre-Entry Course)* ya kujiunga na Chuo, kwa wasichana, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania;
(g) kugharimia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wanataaluma 15 na wafanyakazi waendeshaji 10;

(h) kumalizia upanuzi wa kumbi za kusomea, madarasa na maktaba;

(i) kumalizia ukarabati wa Bweni Na. 2 na kuendeleza ujenzi wa awamu ya pili ya Bweni Na. 3;

(j) kujenga mfumo wa umwagiliaji na mashamba-darasa kwa ajili ya kufundishia Programu ya Uhandisi Ujenzi na Umwagiliaji;

(k) kufanya ukarabati wa karakana na maabara *(Mechanical, Civil, Electrical na Automotive Engineering);*

(l) kukamilisha ujenzi wa jengo la 'Ujenzi na Umwagiliaji';

(m) kuongeza viti na meza zisizohamishika *(fixed chairs and Tables)* katika baadhi ya madarasa ili kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(n) kuendeleza mikakati ya mapambano dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI *(HIV and AIDS)* kwa wanajumuiya wa Chuo; na

(o) kuendeleza ushirikiano na nchi wahisani, Mashirika ya Kimataifa, Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Ufundi vilivyo nchini na vya kimataifa sehemu mbalimbali kama ifuatavyo:

- ushirikiano na Vyuo vya Ufundi barani Afrika chini ya uratibu wa *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa* (CAPA)
- Ushirikiano na Chuo Kikuu cha Camosun cha nchini Canada kupitia mradi wa *Education for Employment* (EFE).
- kushiriki katika mradi wa *Technical Education and Labour Market Support Programme* (TELMS) unaofadhiliwa na Serikali ya Italia
- kushirikiana na wataalamu kutoka Japani katika kufundisha Uhandisi Ujenzi na Umwagiliaji

## VII. SHUKRANI NA PONGEZI

132. **Mheshimiwa Spika**, natoa shukrani za pekee kwa wananchi, viongozi na Wahisani mbalimbali kwa kuchangia utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Baadhi ya Wahisani hao ni Serikali za: Algeria, Canada, China, Cuba, Finland, India, Ireland, Jamhuri ya Watu wa Korea, Japan, Marekani, Misri, Norway, Pakistan, Poland, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Sweden na Uturuki. Aidha, mashirika yaliyochangia katika kufanikisha programu zetu za Elimu ni pamoja na *Aga Khan Education Foundation, Barclays Bank,* Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), CIDA (Canada), COL, CRDB, DAAD, DANIDA, DFID, EDC, GTZ, ILO, *International Reading Association, Irish Aid,* JICA, JOVC, KOICA, NBC, NMB, NORAD, OPEC, *Oxfam, Peace Corps, Plan International,* Sida (Sweden), Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), UNAIDS, UNDP, UNESCO, UNFPA, UNICEF, USAID, VSO, WFP, *Sight Savers International, UNESCO Institute for Life Long Learning* (UIL), *Book Aid International*, BP, *Care International*, CBP, *Children International, Winrock International, World Vision* na ZAIN.

133. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru viongozi wa matawi ya CWT, RAAWU, THTU na TUGHE kwa ushirikiano na ushauri wao katika kushughulikia masuala ya wafanyakazi.

## VIII. MAOMBI YA FEDHA

134. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipitishe makadirio ya matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Jumla ya **Shilingi 659,296,862,000** kwa mwaka wa fedha 2011/12 ili kuiwezesha Wizara kutekeleza Mpango wake. Katika maombi haya:

(a) **Shilingi 71,767,219,156** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Idara ambapo: **Shilingi 34,433,671,000** zinaombwa kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 37,333,548,156** zinaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo;

(b) **Shilingi 452,015,541,460** zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Taasisi. Kati ya hizo**, Shilingi 170,072,086,000** zinaombwa kwa ajili ya mishahara, na **Shilingi 281,939,460,844** zinaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

(c) **Shilingi 135,518,096,000** zinaombwa kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kati ya hizo, **Shilingi 41,098,534,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 94,419,562,000** ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

135. **Mheshimiwa Spika,** nakushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

136. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Kambatisho Na. 1

# Elimu ya Awali

## Uandikishaji kwa Jinsi na Darasa katika Shule za Serikali na zisizo za Serikali, 2007 - 2011

| Type of School and Level of Aggregation | 2007 | | | 2008 | | | | 2009 | | | | 2010 | | | | 2011 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | M | F | T | M | F | T | % Increase | M | F | T | % Increase | M | F | T | % Increase | M | F | T | % Increase |
| Total Govt&Non-Govt (Year I-II) | 387868 | 407143 | 795011 | 435956 | 438025 | 873981 | 9.9 | 445867 | 450279 | 896146 | 2.5 | 461628 | 463837 | 925465 | 3.3 | 538478 | 530730 | 1069208 | 15.5 |
| Total Government (Year I-II) | 377359 | 397954 | 775313 | 400686 | 404721 | 805407 | 3.9 | 422893 | 428191 | 851084 | 5.7 | 440202 | 443465 | 883667 | 3.8 | 502187 | 494894 | 997081 | 12.8 |
| Total Non-Government (Year I-II) | 10509 | 9189 | 19698 | 35270 | 33304 | 68574 | 248.1 | 22974 | 22088 | 45062 | -34.3 | 21426 | 20372 | 41798 | -7.2 | 36291 | 35836 | 72127 | 72.6 |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| Total Year I | 243353 | 267181 | 510534 | 272245 | 276282 | 548527 | 7.4 | 273837 | 280270 | 554107 | 1.0 | 284276 | 289963 | 574239 | 3.6 | 326017 | 316901 | 642918 | 12.0 |
| Government | 236956 | 261686 | 498642 | 251677 | 256580 | 508257 | 1.9 | 260973 | 268008 | 528981 | 4.1 | 272119 | 278281 | 550400 | 4.0 | 305923 | 297085 | 603008 | 9.6 |
| Non Government | 6397 | 5495 | 11892 | 20568 | 19702 | 40270 | 238.6 | 12864 | 12262 | 25126 | -37.6 | 12157 | 11682 | 23839 | -5.1 | 20094 | 19816 | 39910 | 67.4 |
| Total Year II | 144515 | 139962 | 284477 | 163711 | 161743 | 325454 | 14.4 | 172030 | 170009 | 342039 | 5.1 | 177352 | 173874 | 351226 | 2.7 | 212461 | 213829 | 426290 | 21.4 |
| Government | 140403 | 136268 | 276671 | 149009 | 148141 | 297150 | 7.4 | 161920 | 160183 | 322103 | 8.4 | 168083 | 165184 | 333267 | 3.5 | 196264 | 197809 | 394073 | 18.2 |
| Non-Government | 4112 | 3694 | 7806 | 14702 | 13602 | 28304 | 262.6 | 10110 | 9826 | 19936 | -29.6 | 9269 | 8690 | 17959 | -9.9 | 16197 | 16020 | 32217 | 79.4 |

**Tanbihi:** Uandikishaji katika Elimu ya Awali uliongezeka kwa 15.5% kutoka 925,465 mwaka 2010 hadi 1,069 mwaka 2011. Hii inaashiria kuongezeka kwa ushiriki katika Elimu ya Awali.

**Chanzo:** BEST 2011

# Elimu ya Msingi

## Uandikishaji wa Darasa la I - VII kwa Jinsi na Darasa katika Shule za Msingi za Serikali na zisizo za Serikali, 2007 - 2011

| | 2007 | | | 2008 | | | 2009 | | | 2010 | | | 2011 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a) Total Enrol | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| **Std I-VII** | **4215171** | **4101754** | **8316925** | **4261831** | **4148263** | **8410094** | **4248764** | **4192789** | **8441553** | **4203269** | **4216036** | **8419305** | **4159740** | **4203646** | **8363386** |
| Government | 4173825 | 4061607 | 8235432 | 4203180 | 4093428 | 8296608 | 4182915 | 4130165 | 8313080 | 4127500 | 4139526 | 8267026 | 4076899 | 4123752 | 8200651 |
| Non-Govt | 41346 | 40147 | 81493 | 58651 | 54835 | 113486 | 65849 | 62624 | 128473 | 75769 | 76510 | 152279 | 82841 | 79894 | 162735 |
| **b)Total Grades** | | | | | | | | | | | | | | | |
| **Std I** | **699255** | **680038** | **1379293** | **700524** | **679666** | **1380190** | **684388** | **674402** | **1358790** | **681983** | **674591** | **1356574** | **699483** | **688733** | **1388216** |
| Government | 692362 | 673223 | 1365585 | 690766 | 670263 | 1361029 | 673390 | 663952 | 1337342 | 669775 | 662994 | 1332769 | 685671 | 675861 | 1361532 |
| Non-Govt | 6893 | 6815 | 13708 | 9758 | 9403 | 19161 | 10998 | 10450 | 21448 | 12208 | 11597 | 23805 | 13812 | 12872 | 26684 |
| **Std II** | **627349** | **624043** | **1251392** | **655097** | **639170** | **1294267** | **658467** | **653104** | **1311571** | **657297** | **648513** | **1305810** | **650609** | **642097** | **1292706** |
| Government | 620868 | 617567 | 1238435 | 645351 | 630180 | 1275531 | 648135 | 643388 | 1291523 | 644969 | 636888 | 1281857 | 637498 | 629646 | 1267144 |
| Non-Govt | 6481 | 6476 | 12957 | 9746 | 8990 | 18736 | 10332 | 9716 | 20048 | 12328 | 11625 | 23953 | 13111 | 12451 | 25562 |
| **Std III** | **621265** | **613665** | **1234930** | **611985** | **599891** | **1211876** | **649018** | **624368** | **1273386** | **641103** | **638654** | **1279757** | **629929** | **628556** | **1258485** |
| Government | 614769 | 607453 | 1222222 | 602376 | 590965 | 1193341 | 638501 | 614149 | 1252650 | 629044 | 626172 | 1255216 | 616795 | 616155 | 1232950 |
| Non-Govt | 6496 | 6212 | 12708 | 9609 | 8926 | 18535 | 10517 | 10219 | 20736 | 12059 | 12482 | 24541 | 13134 | 12401 | 25535 |
| **Std IV** | **665823** | **655622** | **1321445** | **670453** | **647557** | **1318010** | **592496** | **582367** | **1174863** | **604444** | **602747** | **1207191** | **590442** | **597386** | **1187828** |
| Government | 659280 | 649536 | 1308816 | 661633 | 639318 | 1300951 | 582915 | 572864 | 1155779 | 593147 | 591068 | 1184215 | 578474 | 585232 | 1163706 |
| Non-Govt | 6543 | 6086 | 12629 | 8820 | 8239 | 17059 | 9581 | 9503 | 19084 | 11297 | 11679 | 22976 | 11968 | 12154 | 24122 |
| **Std V** | **593239** | **568340** | **1161579** | **512490** | **507316** | **1019806** | **610857** | **614823** | **1225680** | **551727** | **555546** | **1107273** | **555521** | **561631** | **1117152** |
| Government | 587419 | 562612 | 1150031 | 504401 | 499702 | 1004103 | 601433 | 606123 | 1207556 | 541001 | 544609 | 1085610 | 543746 | 550311 | 1094057 |
| Non-Govt | 5820 | 5728 | 11548 | 8089 | 7614 | 15703 | 9424 | 8700 | 18124 | 10726 | 10937 | 21663 | 11775 | 11320 | 23095 |
| **Std VI** | **589274** | **562458** | **1151732** | **570051** | **550075** | **1120126** | **522027** | **515596** | **1037623** | **601772** | **612396** | **1214168** | **540029** | **550490** | **1090519** |
| Government | 584083 | 557448 | 1141531 | 562855 | 543579 | 1106434 | 513719 | 507679 | 1021398 | 592285 | 602555 | 1194840 | 529518 | 540336 | 1069854 |
| Non-Govt | 5191 | 5010 | 10201 | 7196 | 6496 | 13692 | 8308 | 7917 | 16225 | 9487 | 9841 | 19328 | 10511 | 10154 | 20665 |
| **Std VII** | **418966** | **397588** | **816554** | **541231** | **524588** | **1065819** | **531511** | **528129** | **1059640** | **464943** | **483589** | **948532** | **493727** | **534753** | **1028480** |
| Government | 415044 | 393768 | 808812 | 535798 | 519421 | 1055219 | 524822 | 522010 | 1046832 | 457279 | 475240 | 932519 | 485197 | 526211 | 1011408 |
| Non-Govt | 3922 | 3820 | 7742 | 5433 | 5167 | 10600 | 6689 | 6119 | 12808 | 7664 | 8349 | 16013 | 8530 | 8542 | 17072 |

**Tanbihi:** Uandikishaji katika Shule za Msingi umeshuka kutoka wanafunzi 8,419,305 mwaka 2010 hadi 8,363,386 kwa 0.7% mwaka 2011. Hii inaashiria kuisha kwa malimbikizo ya watoto wote wenye umri wa kwenda shule.

**Chanzo:** BEST 2011

# Elimu ya Sekondari

## Uandikishaji na Walimu katika Shule za Sekondari za Serikali na zisizo za Serikali kwa Jinsi na Darasa, 2007 - 2011

| Name of Indicator and Level of Aggregation | 2007 | | | 2008 | | | 2009 | | | 2010 | | | 2011 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Enrolment | | | | | | | | | | | | | | | |
| a) Form 1 - 6 | | | | | | | | | | | | | | | |
| Total | **543196** | **477314** | **1020510** | **679124** | **543279** | **1222403** | **812945** | **653457** | **1466402** | **910171** | **728528** | **1638699** | **986993** | **802554** | **1789547** |
| Government | 446716 | 382378 | 829094 | 584118 | 451755 | 1035873 | 728322 | 565369 | 1293691 | 792974 | 608356 | 1401330 | 854739 | 660932 | 1515671 |
| Non-Govt | 96480 | 94936 | 191416 | 95006 | 91524 | 186530 | 84623 | 88088 | 172711 | 117197 | 120172 | 237369 | 132254 | 141622 | 273876 |
| b) Form 1 | | | | | | | | | | | | | | | |
| Total | **235539** | **212909** | **448448** | **252116** | **186785** | **438901** | **290696** | **234088** | **524784** | **240017** | **198810** | **438827** | **246487** | **220668** | **467155** |
| Government | 212165 | 188846 | 401011 | 231241 | 164689 | 395930 | 269712 | 210817 | 480529 | 213262 | 168945 | 382207 | 217094 | 186779 | 403873 |
| Non-Govt | 23374 | 24063 | 47437 | 20875 | 22096 | 42971 | 20984 | 23271 | 44255 | 26755 | 29865 | 56620 | 29393 | 33889 | 63282 |
| c) Form 2 | | | | | | | | | | | | | | | |
| **Total** | **137921** | **127066** | **264987** | **200658** | **174967** | **375625** | **196911** | **147604** | **344515** | **254319** | **202427** | **456746** | **252478** | **211451** | **463929** |
| Government | 115306 | 102754 | 218060 | 179289 | 153104 | 332393 | 179436 | 128695 | 308131 | 226782 | 172088 | 398870 | 220738 | 175986 | 396724 |
| Non-Govt | 22615 | 24312 | 46927 | 21369 | 21863 | 43232 | 17475 | 18909 | 36384 | 27537 | 30339 | 57876 | 31740 | 35465 | 67205 |
| d) Form 3 | | | | | | | | | | | | | | | |
| **Total** | **80403** | **66707** | **147110** | **117568** | **100962** | **218530** | **177706** | **153138** | **330844** | **195222** | **149075** | **344297** | **246852** | **199535** | **446387** |
| Government | 59630 | 46140 | 105770 | 96190 | 79163 | 175353 | 159789 | 133991 | 293780 | 170704 | 122815 | 293519 | 215239 | 165289 | 380528 |
| Non-Govt | 20773 | 20567 | 41340 | 21378 | 21799 | 43177 | 17917 | 19147 | 37064 | 24518 | 26260 | 50778 | 31613 | 34246 | 65859 |
| e) Form 4 | | | | | | | | | | | | | | | |
| **Total** | **57553** | **48989** | **106542** | **73675** | **57519** | **131194** | **109205** | **92211** | **201416** | **177176** | **149639** | **326815** | **190186** | **143452** | **333638** |
| Government | 39609 | 31187 | 70796 | 54898 | 40316 | 95214 | 92568 | 74787 | 167355 | 153867 | 126128 | 279995 | 163838 | 115279 | 279117 |
| Non-Govt | 17944 | 17802 | 35746 | 18777 | 17203 | 35980 | 16637 | 17424 | 34061 | 23309 | 23511 | 46820 | 26348 | 28173 | 54521 |

### Kiambatisho Na. 3 - kinaendelea

| Name of Indicator and Le | 2007 | | | 2008 | | | 2009 | | | 2010 | | | 2011 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| f) Form 5 | | | | | | | | | | | | | | | |
| Total | **19778** | **13310** | **33088** | **21949** | **15867** | **37816** | **25182** | **17870** | **43052** | **23056** | **15278** | **38334** | **27088** | **14260** | **41348** |
| Government | 13151 | 8638 | 21789 | 14475 | 10765 | 25240 | 18604 | 12597 | 31201 | 15782 | 10283 | 26065 | 20992 | 9273 | 30265 |
| Non-Govt | 6627 | 4672 | 11299 | 7474 | 5102 | 12576 | 6578 | 5273 | 11851 | 7274 | 4995 | 12269 | 6096 | 4987 | 11083 |
| g) Form 6 | | | | | | | | | | | | | | | |
| Total | **12002** | **8333** | **20335** | **13158** | **7179** | **20337** | **13245** | **8546** | **21791** | **20381** | **13299** | **33680** | **23902** | **13188** | **37090** |
| Government | 6855 | 4813 | 11668 | 8025 | 3718 | 11743 | 8213 | 4482 | 12695 | 12577 | 8097 | 20674 | 16838 | 8326 | 25164 |
| Non-Govt | 5147 | 3520 | 8667 | 5133 | 3461 | 8594 | 5032 | 4064 | 9096 | 7804 | 5202 | 13006 | 7064 | 4862 | 11926 |
| h) Form 1 - 4 | | | | | | | | | | | | | | | |
| Total | **511416** | **455671** | **967087** | **644017** | **520233** | **1164250** | **774518** | **627041** | **1401559** | **866734** | **699951** | **1566685** | **936003** | **775106** | **1711109** |
| Government | 426710 | 368927 | 795637 | 561618 | 437272 | 998890 | 701505 | 548290 | 1249795 | 764615 | 589976 | 1354591 | 816909 | 643333 | 1460242 |
| Non-Govt | 84706 | 86744 | 171450 | 82399 | 82961 | 165360 | 73013 | 78751 | 151764 | 102119 | 109975 | 212094 | 119094 | 131773 | 250867 |
| i) Form 5 - 6 | | | | | | | | | | | | | | | |
| Total | **31780** | **21643** | **53423** | **35107** | **23046** | **58153** | **38427** | **26416** | **64843** | **43437** | **28577** | **72014** | **50990** | **27448** | **78438** |
| Government | 20006 | 13451 | 33457 | 22500 | 14483 | 36983 | 26817 | 17079 | 43896 | 28359 | 18380 | 46739 | 37830 | 17599 | 55429 |
| Non-Govt | 11774 | 8192 | 19966 | 12607 | 8563 | 21170 | 11610 | 9337 | 20947 | 15078 | 10197 | 25275 | 13160 | 9849 | 23009 |
| j)Teaching Staff | | | | | | | | | | | | | | | |
| Total | **16316** | **6936** | **23252** | **23122** | **9713** | **32835** | **22972** | **10982** | **33954** | **27821** | **12696** | **40517** | **36357** | **15789** | **52146** |
| Government | 10534 | 5377 | 15911 | 16790 | 8181 | 24971 | 17240 | 9192 | 26432 | 19666 | 10586 | 30252 | 26635 | 13299 | 39934 |
| Non-Govt | 5782 | 1559 | 7341 | 6332 | 1532 | 7864 | 5732 | 1790 | 7522 | 8155 | 2110 | 10265 | 9722 | 2490 | 12212 |

**Tanbihi:** Kumekuwa na ongezeo la uandikishaji katika Kidato cha 1-6 kwa 75% kutoka wanafunzi 1,020,510 mwaka 2007 hadi 1,789,547 mwaka 2011. Hii inatokana na juhudi za serikali za kujenga angalau shule moja katika kila kata nchini. Uandikishaji katika Shule za Sekondari za Serikali umeongezeka kwa 82% kutoka 829,094 mwaka 2006 hadi 1,515,671 mwaka 2011.

**Chanzo:** BEST 2011

Kiambatisho Namba 4

# Elimu ya Ualimu

## Udahili katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali kwa Madaraja na Nyanja za Kitaalamu 2008 - 2011

| Year | Type | Fields of Study – Diploma – Sciences | | | Arts | | | Special Education | | | Grand Total | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| 2008 | Govt | 3290 | 1899 | **5189** | 5764 | 5436 | **11200** | 151 | 140 | **291** | 9205 | 7475 | **16680** |
| | Non-Govt | 927 | 950 | **1877** | 1309 | 2002 | **3311** | 0 | 0 | **0** | 2236 | 2952 | **5188** |
| | **Total** | **4217** | **2849** | **7066** | **7073** | **7438** | **14511** | **151** | **140** | **291** | **9205** | **7475** | **21868** |
| **Percentage** | | **19.3** | **13.0** | **32.3** | **32.3** | **34.0** | **194.1** | **2.0** | **1.9** | **3.9** | **42.1** | **34.2** | **100.0** |
| 2009 | Govt | 4901 | 2694 | **7595** | 1807 | 995 | **13979** | 64 | 51 | 115 | 12389 | 9300 | **21689** |
| | Non-Govt | 2542 | 3054 | **5596** | 3312 | 4913 | **8225** | 13 | 10 | 23 | 5867 | 7977 | **13844** |
| | **Total** | **7443** | **5748** | **13191** | **5119** | **5908** | **22204** | **77** | **61** | **138** | **18256** | **17277** | **35533** |
| **Percentage** | | **20.9** | **16.2** | **37.1** | **14.4** | **16.6** | **128.5** | **0.4** | **0.4** | **0.8** | **51.4** | **48.6** | **100.0** |
| 2010 | Govt | 6350 | 4780 | **11130** | 5764 | 6379 | **14393** | 214 | 77 | 291 | 14578 | 11236 | **25814** |
| | Non-Govt | 3038 | 1992 | **5030** | 5764 | 3369 | **5804** | 0 | 0 | 0 | 5473 | 5361 | **10834** |
| | **Total** | **9388** | **6772** | **16160** | **5764** | **9748** | **20197** | **214** | **77** | **291** | **20051** | **16597** | **36648** |
| **Percentage** | | **25.6** | **18.5** | **44.1** | **15.7** | **26.6** | **121.7** | **1.3** | **0.5** | **1.8** | **54.7** | **45.3** | **100.0** |

| 2011 | Type | Diploma – Sciences | | | Arts | | | Total | | | Certificate – Grade A | | | Special Education | | | Pre-Primary Education | | | Sports | | | Grand Total | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| | | 2256 | 1119 | **3375** | 5153 | 3860 | **9013** | 7409 | 4979 | **12388** | 5924 | 5483 | **11407** | 207 | 153 | **360** | 0 | 0 | **0** | 51 | 37 | **88** | 13591 | 10652 | **24243** |
| | Non-Govt | 318 | 320 | **638** | 1215 | 1158 | **2373** | 1533 | 1478 | **3011** | 5136 | 5036 | **10172** | 110 | 71 | **181** | 15 | 76 | **91** | 0 | 0 | **0** | 6794 | 6661 | **13455** |
| | **Total** | **2574** | **1439** | **4013** | **6368** | **5018** | **11386** | **8942** | **6457** | **15399** | **11060** | **10519** | **21579** | **317** | **224** | **541** | **15** | **76** | **91** | **51** | **37** | **88** | **20385** | **17313** | **37698** |
| **Percentage** | | **14.9** | **8.3** | **23.2** | **36.8** | **29.0** | **65.8** | **51.6** | **37.3** | **88.9** | **63.9** | **60.8** | **124.6** | **1.8** | **1.3** | **3.1** | **0.1** | **0.4** | **0.5** | **0.3** | **0.2** | **0.5** | **117.7** | **100.0** | **217.7** |

**Tanbihi:** Udahili katika Vyuo vya Serikali na visivyo vya Serikali ulikuwa walimu wanafunzi 37,698. Udahili katika nyanja za Sayansi ulikuwa 10.6%, Sanaa 30.2% na Elimu Maalum 1.4%.

**Chanzo:** BEST 2011

Kiambatisho Na.5

# Elimu ya Ufundi

## Udahili katika Vyuo vya Ufundi kwa Nyanja za Kitaaluma Mwaka 2010

| Field of Study | Certificate | | | Ordinary Diploma | | | Advanced Diploma | | | Higher Diploma | | | Bachelor Degree | | | Post Graduate Certificate | | | Post Graduate Diploma | | | Masters | | | Grand Total | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Agriculture | 2713 | 1517 | **4230** | 1332 | 408 | **1740** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 4045 | 1925 | **5970** |
| Education | 16 | 65 | **81** | 182 | 243 | **425** | 47 | 61 | **108** | 0 | 0 | **0** | 99 | 97 | **196** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 344 | 466 | **810** |
| Engineering, Manufacturing and Construction | 1015 | 268 | **1283** | 2431 | 253 | **2684** | 0 | 0 | **0** | 23 | 2 | **25** | 1710 | 142 | **1852** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 5179 | 665 | **5844** |
| Health and Welfare | 1444 | 3261 | **4705** | 1887 | 3465 | **5352** | 345 | 217 | **562** | 26 | 30 | **56** | 177 | 476 | **653** | 0 | 0 | **0** | 8 | 14 | **22** | 0 | 0 | **0** | 3887 | 7463 | **11350** |
| Humanities and Arts | 46 | 31 | **77** | 104 | 44 | **148** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 150 | 75 | **225** |
| Science | 1726 | 452 | **2178** | 1590 | 424 | **2014** | 650 | 215 | **865** | 763 | 151 | **914** | 1407 | 263 | **1670** | 0 | 0 | **0** | 11 | 2 | **13** | 23 | 8 | **31** | 6170 | 1515 | **7685** |
| Services | 752 | 701 | **1453** | 196 | 77 | **273** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 35 | 8 | **43** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 983 | 786 | **1769** |
| Social Sciences, Business and Law | 7640 | 11058 | **18698** | 6958 | 7980 | **14938** | 1651 | 1054 | **2705** | 1926 | 1066 | **2992** | 4390 | 3132 | **7522** | 95 | 28 | **123** | 851 | 505 | **1356** | 2073 | 980 | **3053** | 25584 | 25803 | **51387** |
| **Grand Total** | **15352** | **17353** | **32705** | **14680** | **12894** | **27574** | **2693** | **1547** | **4240** | **2738** | **1249** | **3987** | **7818** | **4118** | **11936** | **95** | **28** | **123** | **870** | **521** | **1391** | **2096** | **988** | **3084** | **46342** | **38698** | **85040** |
| **Percentage(%)** | **18.1** | **20.4** | **38.5** | **17.3** | **15.2** | **32.4** | **3.2** | **1.8** | **5.0** | **3.2** | **1.5** | **4.7** | **9.2** | **4.8** | **14.0** | **0.1** | **0.0** | **0.1** | **1.0** | **0.6** | **1.6** | **2.5** | **1.2** | **3.6** | **54.5** | **45.5** | **100.0** |

**Tanbihi:** Programu zisizo za Shahada zinachukua 80.7% ikilinganishwa na 19.3% ya programu za shahada. Idadi kubwa ya wanachuo katika programu zisizokuwa za shahada (70.9%) wanachukua mafunzo ya cheti na diploma za kawaida. Wachache tu (9.7%) wanachukua mafunzo ya diploma za juu au za uzamili.

**Chanzo:** BEST 2011

# Kiambatisho Na. 6

**ELIMU YA JUU**

**UDAHILI KATIKA VYUO VIKUU NA VYUO VIKUU VISHIRIKI VYA SERIKALI NA VISIVYO VYA SERIKALI KWA VIWANGO NA JINSI, 2010/11**

| Jina la Chuo | KOZI ZISIZO ZA SHAHADA | | | | | | | | | | | | KOZI ZA SHAHADA | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Certificate | | | Ordinary Diploma | | | Advanced Diploma | | | Higher Diploma | | | Bachelor | | | Post Graduate Certificate | | | Post Graduate Diploma | | | Masters | | | Doctorate | | | Grand Total | | |
| | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| AKU | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 18 | 24 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 34 | 24 | 58 | 0 | 0 | 0 | 40 | 42 | 82 |
| ARU | 0 | 1 | 1 | 11 | 3 | 14 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1850 | 688 | 2538 | 0 | 0 | 0 | 22 | 1 | 23 | 85 | 18 | 103 | 10 | 3 | 13 | 1978 | 714 | 2692 |
| DUCE | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1569 | 1324 | 2893 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1569 | 1324 | 2893 |
| HKMU | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 202 | 222 | 424 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 | 5 | 20 | 0 | 0 | 0 | 217 | 227 | 444 |
| IMTU | 17 | 21 | 38 | 1 | 32 | 33 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 586 | 299 | 885 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 | 6 | 20 | 0 | 0 | 0 | 618 | 358 | 976 |
| IUCO | 27 | 22 | 49 | 53 | 42 | 95 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1706 | 1267 | 2973 | 0 | 0 | 0 | 18 | 5 | 23 | 113 | 53 | 166 | 0 | 0 | 0 | 1917 | 1389 | 3306 |
| KCMC | 0 | 0 | 0 | 37 | 39 | 76 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 489 | 334 | 823 | 0 | 0 | 0 | 74 | 27 | 101 | 20 | 14 | 34 | 6 | 6 | 12 | 626 | 420 | 1046 |
| KIU | 116 | 134 | 250 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 80 | 68 | 148 | 444 | 329 | 773 | 0 | 1 | 1 | 38 | 7 | 45 | 44 | 17 | 61 | 0 | 0 | 0 | 722 | 558 | 1280 |
| MMU | 0 | 0 | 0 | 199 | 273 | 472 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 405 | 309 | 714 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 24 | 18 | 42 | 0 | 0 | 0 | 628 | 600 | 1228 |
| MU | 129 | 115 | 244 | 100 | 91 | 191 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1203 | 987 | 2190 | 0 | 0 | 0 | 513 | 441 | 954 | 605 | 311 | 916 | 13 | 2 | 15 | 2563 | 1947 | 4510 |
| MUCCOBS | 315 | 315 | 630 | 360 | 314 | 674 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1135 | 675 | 1810 | 0 | 0 | 0 | 28 | 20 | 48 | 21 | 4 | 25 | 0 | 0 | 0 | 1859 | 1328 | 3187 |
| MUCE | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1062 | 905 | 1967 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1062 | 905 | 1967 |
| MUCO | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1010 | 816 | 1826 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 28 | 15 | 43 | 1 | | 1 | 1040 | 831 | 1871 |
| MUHAS | 41 | 28 | 69 | 400 | 330 | 730 | 31 | 17 | 48 | 0 | 0 | 0 | 1072 | 368 | 1440 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 245 | 151 | 396 | 0 | 0 | 0 | 1789 | 894 | 2683 |
| MUM | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 557 | 372 | 929 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 557 | 372 | 929 |
| MWUCE | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 210 | 134 | 344 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 210 | 134 | 344 |
| OUT | 6084 | 3778 | 9862 | 1028 | 710 | 1738 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 19678 | 7580 | 27258 | 0 | 0 | 0 | 426 | 161 | 587 | 3456 | 1247 | 4703 | 100 | 24 | 124 | 30772 | 13500 | 44272 |
| RUCO | 131 | 186 | 317 | 135 | 100 | 235 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 966 | 495 | 1461 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1232 | 782 | 2014 |
| SAUT | 304 | 334 | 638 | 0 | 0 | 0 | 267 | 204 | 471 | 0 | 0 | 0 | 5504 | 4186 | 9690 | 0 | 0 | 0 | 21 | 15 | 36 | 184 | 99 | 283 | 12 | 4 | 16 | 6292 | 4842 | 11134 |
| SJUT | 66 | 77 | 143 | 251 | 217 | 468 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1874 | 1530 | 3404 | 0 | 0 | 0 | 58 | 69 | 127 | 38 | 19 | 57 | 0 | 0 | 0 | 2287 | 1912 | 4199 |
| SUA | 2 | 1 | 3 | 0 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3352 | 1305 | 4657 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3354 | 1306 | 4660 |
| SUZA | 13 | 6 | 19 | 184 | 312 | 496 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 500 | 378 | 878 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 697 | 696 | 1393 |
| TEKU | 25 | 27 | 52 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2271 | 1257 | 3528 | 0 | 0 | 0 | 16 | 0 | 16 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2312 | 1284 | 3596 |
| TUDARCO | 96 | 80 | 176 | 6 | 9 | 15 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 949 | 823 | 1772 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1051 | 912 | 1963 |
| UDOM | 3 | 1 | 4 | 6 | 1 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12232 | 6185 | 18417 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 780 | 341 | 1121 | 24 | 9 | 33 | 13046 | 6538 | 19584 |
| UDSM | 2 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7513 | 4258 | 11771 | 495 | 158 | 653 | 0 | 0 | 0 | 2314 | 1260 | 3574 | 202 | 86 | 288 | 10526 | 5763 | 16289 |
| UoA | 0 | 0 | 0 | 6 | 16 | 22 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 709 | 365 | 1074 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 715 | 381 | 1096 |
| GRAND TOTAL | 7372 | 5127 | 12499 | 2777 | 2491 | 5268 | 298 | 221 | 519 | 80 | 68 | 148 | 69054 | 37409 | 106463 | 495 | 159 | 654 | 1215 | 748 | 1963 | 8020 | 3602 | 11622 | 368 | 134 | 502 | 89679 | 49959 | 139638 |

Kiambatisho Na. 7

# UKAGUZI WA SHULE

## Idadi ya Taasisi Zilizokaguliwa Mwaka 2010/2011

| Taasisi/Kundi | Taasisi zilizokuwepo hadi Juni 2011 | Idadi ya Taasisi Zilizopangwa Kukaguliwa | Taasisi Zilizokaguliwa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Madarasa ya Elimu ya Awali | 40730 | 5450 | 2473 | 45.4 |
| Shule za Msingi | 16001 | 3375 | 1276 | 37.8 |
| Vituo vya Ufundi Stadi vya Waliomaliza Elimu ya Msingi | 358 | 170 | 55 | 32.4 |
| Shule/Vitengo vya Elimu Maalum | 354 | 140 | 40 | 28.6 |
| Vituo vya Elimu Maalum | 18557 | 4328 | 1296 | 29.9 |
| Shule za Sekondari | 4367 | 1430 | 1035 | 72.4 |
| Vyuo vya Ualimu | 103 | 93 | 40 | 43.0 |

**Chanzo** Taarifa za Ukaguzi wa Shule Mwaka 2010/11.